# Nipashe

Alhamisi Julai 16, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580285

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Kishindo mapokezi Dk. Mwinyi Zanzibar, mwenyewe atoa neno

UKURASA 3




UKURASA 11

# Vigogo zaidi wajitosa CCM



• **Wamo** Majaliwa, Wasira na Salma Kikwete, watoto wa viongozi mashuhuri wachomoza, waandishi, wasanii nao wamiminika, bosi TIC aibukia Masasi... *Endelea Uk. 2,3,4,7,19*



Jacob Tesha
**Moshi Vijijini**



Benjamin Sitta
**Kawe**



Salma Kikwete
**Mchinga**



Stephen Wassira
**Bunda Mjini**



Paul Makonda
**Kigamboni**



Frida Rweyemamu
**Bumbuli**



Geoffrey Mwambe
**Masasi**



Angel Akilimali
**Segerea**


Nipashe MWANGA WA JAMII

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE






Gazeti la Nipashe linatoa fursa kwa wagombea wote wa vyama vya siasa kunadi sera zao kupitia kurasa zetu kwa gharama nafuu.

Wasiliana nasi
The Guardian Limited
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


## JPM amtumbua Makonda Dar

UK. 4


**MICHEZO** TFF YAMTETEA MORRISON, YAIACHIA YANGA IAMUE UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Matokeo kura za maoni CHADEMA yashtua wengi

**Na Elizabeth Zaya**

MATOKEO ya kura za maoni ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), yameendelea kushtua kutokana na makada wanawake wa chama hicho kuibuka washindi katika maeneo mengi.

Katika kura hizo zilizoanza kupigwa mwanzoni mwa wiki, wabunge waliomaliza muda wao katika Bunge lililopita kupitia chama hicho, wameibuka washindi.

Kwa matokeo yaliyotangazwa jana, waliong`ara katika kura za maoni ni Lucy Owenya (Moshi Vijijini) ambaye pia ameshinda kwenye kipengele cha ubunge viti maalum kwenye jimbo hilohilo.

Mwingine ni aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Geita katika Bunge la 11, Upendo Peneza, ambaye ameshinda kwenye kura za maoni kuwania ubunge wa Jimbo la Geita Mjini.

Katika Jimbo la Same Mashariki mkoani Kilimanjaro, aliyekuwa mbunge wake katika Bunge lililopita, Nagwenjwa Kaboyoka, ameshinda katika kura hizo kuwania tena ubunge.

Kaboyoka, ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) katika Bunge lililopita, ameibuka mshindi katika kura za kumsaka mbunge wa viti maalum kwenye jimbo hilo.

Rebeka Mngodo ametangazwa mshindi katika kura za maoni kuiwakilisha CHADEMA kusaka ubunge wa Arumeru Mashariki huku mwandishi wa habari, Devotha Minja, aking'ara katika kumtafuta mgombea wa ubunge kupitia chama hicho kwenye Morogoro Mjini.

Devotha, ambaye alikuwa mbunge wa viti maalum katika Bunge lililopita, pia ameshinda kura za maoni kumsaka mbunge wa viti maalum kwenye jimbo hilo. Katika Jimbo la Mbozi mkoani Songwe, aliyekuwa mbunge wake, Pascal Haonga, alitangazwa mshindi kwenye kura za maoni huku Ezekiel Wenje akiibuka mshindi kwenye Jimbo la Rorya.

Jumanne Sunta alitangazwa mshindi katia kura za maoni Jimbo la Manyoni Magharibi wakati Anipher Chiwili aliibuka mshindi kwenye Jimbo la Rufiji.

Aden Mayala aliibua kidedea kwenye kura hizo Jimbo la Songea Mjini huku Stella Mapunda akitangazwa mshindi wakati wa kumsaka mbunge wa viti maalum katika jimbo hilo.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwapungia mkono wananchi mbalimbali waliojipanga barabarani akiwa katika msafara, wakati wa mapokezi yake baada ya kuwasili mjini Zanzibar jana, akitokea jijini Dodoma. **HABARI UK. 3. PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Vigogo zaidi CCM wajitosa ubunge

**Na Waandishi Wetu**

VIGOGO mbalimbali waliokuwapo kwenye serikali zilizopita na ya sasa, wamejitokeza kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya kupitishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupeperusha bendera katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Miongoni mwao ni Salma Kikwete, mke wa Rais mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete anayewania Jimbo la Lindi Mjini. Wengine waliojitosa ni watoto wa viongozi walioshika nafasi za juu katika serikali ya awamu ya kwanza hadi ya nne.

Wanachama wa CCM walioko madarakani ni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliyechukua Jimbo la Ruangwa, huku Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akijitosa Kigamboni.

Watoto wa vigogo waliochukua ni aliyekuwa Meya wa Kinondoni, Benjamin Sitta ambaye mtoto wa Samuel Sitta, spika wa zamani wa Bunge la Tanzania anayewania Kawe, Mtoto wa Waziri Mkuu mstaafu John Malecela, aitwaye Samwel Malecela. Wengine ni Masache Kasaka, mtoto wa aliyekuwa mwanasiasa mkongwe, Njelu Kasaka. Katika orodha ya watu hao mashuhuri yumo pia aliyekuwa Waziri na Mkuu wa Mkoa katika serikali za awamu ya kwanza, ya pili na ya nne, Stephen Wassira ambaye anatupa karata yake Bunda Mjini.

Waliokuwa wabunge miaka mitano iliyopita nao walijitokeza kuomba ridhaa ya kupeperusha bendera ya chama hicho, Bona Kamoli amechukua Segerea na Kangi Lugola Jimbo la Mwibara.

Wengine ni aliyekuwa Mbunge wa Kinondoni hadi mwaka 2015, Idd Azan, aliyekuwa Mbunge wa Mbagala, Issa Mangungu, Abdalah Mtulia (Temeke) mbunge wa zamani wa Kigamboni, Mwinchoum Msomi.

Pia Salome Komba, mjane wa msanii na aliyekuwa Mbunge wa Mbinga na baadaye Nyasa, marehemu John Komba, aitwaye Salome Komba, akiomba ridhaa Jimbo la Kawe.

Aidha, Kiongozi wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima ameungana na mdogo wake Wakili Methusela Gwajima katika kinyang'anyiro kwenye Jimbo la Kawe.

Naye Meya mstaafu wa Temeke, Abdallah Chaurembo, amejitokeza kuomba ubunge katika Jimbo la Temeke na Ansar Kachwamba Jimbo la Kigamboni.

Wengine waliojitokeza ni waandishi wa habari, akiwamo Mkuu wa Idara Siasa na Habari wa vyombo vya habari vya CCM, Angela Akilimali, anayeomba ubunge Jimbo la Ukonga. Pia yumo Makamu wa Rais wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Jane Mihanji, anawania Jimbo la Mlimba na Mwandishi wa Habari wa TBC, Enock Bwigane amechukua Jimbo la Busokelo.

Wengine ni Mtangazaji wa Channel Ten, Hamisi Mkotya, Mwandishi wa Habari wa Uhuru, Shakira Nyerere, Mtangazaji wa Azam, Baruan Muhuza, wamechukua fomu kuwania majimbo ya Kigoma Mjini.

Wengine ni Mwanasheria wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira Tanzania (NEMC), Manchare Suguta Jimbo la Tarime Mjini na Anne Kilango Malecela, mke wa Waziri Mkuu mstaafu, amechukua Jimbo la Same Mashariki.

Pia wamo aliyekuwa Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dk. Elisha Osati (Mbagala), wasanii mbalimbali akiwamo Msanii Master Jay (Joachim Kimario) Jimbo la Rombo na Msanii MC Pilipili (Emmanuel Mathias) Jimbo la Bahi.

# Mnyika aanika sababu kuachia Jimbo la Kibamba

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, ametaja sababu zilizomsukuma kutogombea tena ubunge jimbo la Kibamba katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu.

Kupitia akaunti yake ya Twitter, Mnyika aliandika jana kuwa: "Nyerere aliwahi kuachia uwaziri mkuu akabaki kuimarisha TANU, nami sitagombea ubunge 2020, nitumikie ipasavyo ukatibu mkuu CHADEMA, tushinde uchaguzi tulete mabadiliko."

Mnyika amekuwa mbunge wa Jimbo la Kibamba kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2015.

Mwaka 2010 hadi 2015 alikuwa mbunge kupitia jimbo la Ubungo na baada ya jimbo hilo kugawanywa na kupatikana Ubungo na Kibamba, ndipo mwaka 2015 alipogombea KIbamba na kupata ridhaa hiyo.

Mnyika aliteuliwa kuwa katibu mkuu wa CHADEMA mapema mwaka huu kuchukua nafasi ya Dk. Vincent Mashinji, ambaye baada ya kuondolewa alijiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Juzi, katika kura za maoni za ubunge kupitia CHADEMA zilizoendeshwa kwenye jimbo hilo la Kibamba, Ernest Mgawe alishinda kwa kupata kura 30 kati ya 71 za Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo.

Wengine waliogombea ni Names Tarimo aliyepata kura 22 na Humphrey Sambo kura 19.

# Kishindo mapokezi Dk. Mwinyi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Hussein Mwinyi, jana alipata mapokezi ya kishindo kutoka kwa wanachama wa chama hicho, alipowasili Zanzibar.

Mgombea huyo ambaye aliteuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa CCM jijini Dodoma Ijumaa kisha kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa chama hicho Jumamosi, aliwasili Zanzibar akitokea jijini Dodoma, vilikofanyika vikao vya CCM.

Dk. Mwinyi alipokelewa na umati uliojitokeza kumpokea katika Uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume hadi ofisi kuu za CCM Kisiwandui.

Mapokezi hayo yalisababisha baadhi ya huduma za kijamii kusimama kwa takribani saa tatu kupisha ujio wa mgombea huyo, huku rangi za kijani na njano zikiwa zimetanda katika maeneo mbalimbali ya mji wa Zanzibar. Mapokezi hayo yalipambwa na burudani mbalimbali za ngoma za asili, taarabu na wasanii wa muziki wa kizazi kipya kutoka Zanzibar na Tanzania Bara, akiwamo msanii Ali Kiba alietumbuiza.

Dk. Mwinyi aliwasili uwanja wa ndege majira ya saa 5:30 asubuhi ambapo alitembea kwa gari la wazi na kuwasili Kisiwandui saa 7:00 mchana.

Baada ya kufika ofisi kuu za CCM alizuru kaburi la Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume na kupata tambiko kutoka kwa wazee wa CCM.

**SHEIN AMNADI**

Akimtambulisha mgombea huyo kwa wanachama wa CCM, Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema Dk. Mwinyi ni mzaliwa wa Zanzibar na wale wanaosema kuwa sio kwao Zanzibar waache kasumba hizo.

Aliwataka baadhi ya wananchi na wanasiasa kuacha kufanya siasa za 'kufilisika' kwa kumchafua mgombea wa urais wa Zanzibar kwa kumhusisha na mambo ambayo hayamhusu.

Alieleza kuwa Mwinyi ana sifa zote za kuwa Rais wa Zanzibar pia ni mtu mtiifu, mwadilifu mwenye hekima na busara.

**MWINYI ATOA NENO**

Kwa upande wake, Dk. Mwinyi aliahidi kuendeleza na kuimarisha umoja wa kitaifa wa Wazanzibari wote na kuyalinda Mapinduzi na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema umoja na kitaifa ndiyo tunu ya taifa la Zanzibar, na kwamba hatawavumilia watu wenye nia ya kudhoofisha mambo ya msingi yanayowaunganisha wananchi wa visiwa hivyo.

"Nimefanya maamuzi ya kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa wananchi wote bila ubaguzi... nataka kubadilisha maisha ya Wazanzibari kuwa bora," alisema.

Alisema ataiongoza Zanzibar kwa misingi ya katiba na sheria, na kuwa wabadhirifu, wazembe na wala rushwa hawana nafasi katika Serikali yake huku akiahidi kuona kero hizo zinatokomezwa.

# Makada 8 CCM wamvaa Ndugai ubunge Kongwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAKADA tisa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamejitokeza kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya kuteuliwa kuwania ubunge wa Kongwa kupitia chama hicho katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, akiwamo Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Tangu kufunguliwa kwa dirisha la uchukuaji fomu juzi, mbali na Spika Ndugai, makada wengine wa chama hicho waliokuwa wamejitosa kwenye jimbo hilo hadi jana ni Moris Zaidi, Dk. Samora Mshang'a, Apiov Lywiwa, Dk. Philemon Saigodi, Dotto Chibupa, Martin Chihimba na Sehewa Elias.

Katika Jimbo la Chemba, makada 27 wa CCM walikuwa wamechukua fomu hadi jana, akiwamo aliyekuwa mbunge wake, Juma Nkamia, Mwandishi wa Habari na Mtangazaji wa Channel Ten, Hamisi Mkotya, na Mwandishi wa Habari wa Uhuru, Shakira Nyerere. Kati yao, sita wamesharejesha fomu.

Jimbo la Mpwapwa hadi jana lilikuwa na makada 48 waliokuwa wamejitokeza kuchukua fomu, akiwamo aliyekuwa mbunge wake wa muda mrefu, George Lubeleje.

Kwenye Jimbo la Kibakwe, hadi jana kulikuwa na wanachama 15 wa CCM waliokuwa wamechukua fomu, akiwamo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene.

Pia, wanachama 10 walikuwa wamechukua fomu hadi jana jioni kuomba kuwania Jimbo la Kondoa, akiwamo Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Ashatu Kijaji, ambaye anatetea nafasi yake na amerejesha fomu.

Katika Jimbo la Kondoa Mjini, hadi jana walikuwa wamejitokeza wanachama 40. Kati yao, 10 wamerejesha fomu akiwamo aliyekuwa mbunge wake, Edwin Sanda.

Makada 30 walikuwa wamechukua fomu kuwania nafasi Jimbo la Bahi, akiwamo mchekeshaji Emmanuel Mathias, maarufu MC Pilipili, huku kukiwa na makada 40 waliojitokeza Jimbo la Dodoma Mjini, akiwamo aliyewahi kuwa mbunge wake mwaka 2010 na aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dodoma, Robert Mwinje.

Katika Jimbo la Chilonwa, walikuwa wamejitokeza wanachama 26 hadi jana, akiwamo aliyekuwa mbunge wake katika Bunge lililopita, Joel Mwaka na mtoto wa Waziri Mkuu mstaafu, Samwel Malecela.

Jimbo la Mtera lilikuwa limewavuta wanachama 17 wa CCM hadi jana akiwamo alikuwa mbunge wake, Livingstone Lusinde, huku kukiwa na wanachama wanawake 75 waliojitokeza kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya kuteuliwa ubunge viti maalum kupitia Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT) Mkoa wa Dodoma.



# Watu wenye ulemavu wahimizwa kugombea

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SHIRIKISHO la Watu wenye Ulemavu Tanzania Mkoa wa Morogoro, limewataka wanachama wake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na Rais unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Oscar Changala, wakati akizungumza na wanahabari mjini Morogoro kuhusu mchakato wa uchukuaji wa fomu za wagombea kwa vyama mbalimbali vinavyotarajia kusimamisha wagombea kwenye uchaguzi huo.

Alisema shirikisho limejipanga kutoa elimu na hamasa kwa kundi hilo ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuchagua na kuchaguliwa kwenye nafasi mbalimbali.

Changala, alisema watu wenye ulemavu wana haki sawa kushiriki katika kuchagua na kuchaguliwa sawa na watu wengine wasio na ulemavu.

Mmoja wa watiania ya ubunge wa wa viti malaumu kupitia kundi watu wenye ulemavu, Pano Kashu, alisema wenye ulemavu wasiogope kuomba nafasi za kuchaguliwa kwa nafasi ya ubunge, udiwani na urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Kashu, alimpongeza Rais John Magufuli ambaye amekuwa akiliangalia kundi hilo, na kwamba kwa sasa wamejawa na matumaini ya kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Wenye ulemavu tuna haki na wajibu wetu kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu kuomba nafasi za uongozi ukiwamo udiwani na ubunge kwa vile tuna uwezo mkubwa wa kuongoza na hata kuwazidi wasio na ulemavu," alisema Kashu.

Kashu alisema mazingira ya uchaguzi wa mwaka huu yana mwelekeo wa kuwa huru na haki, na yanatoa fursa sawa kwa watu wenye ulemavu watakaojitokeza kuomba nafasi za kuchaguliwa sawa na watu wengine.



Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, alipowasili kwa baiskeli katika ofisi za CCM Songea Mjini kuchukua fomu ya kuwania tena ubunge wa Jimbo la Songea Mjini jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC wa Dodoma ajitosa ubunge Shinyanga Mjini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAKADA 48 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamejitosa kuchukua fomu kuomba ridhaa ya kuteuliwa kuwania kiti cha ubunge wa Shinyanga Mjini kupitia chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Kwenye orodha hiyo ndefu ya makada wa chama hicho, yumo Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Stephen Masele.

Juzi makada 30 walichukua fomu za kuomba ridhaa ya CCM kuwania ubunge katika jimbo hilo wakiongozwa na Masele na jana makada wengine 18, akiwamo Katambi, walijitokeza kuchukua fomu kusaka nafasi kwenye jimbo hilo.

Mbali na Katambi, makada wengine wa CCM waliojitokeza jana ni pamoja na Joseph Kimaro, Isack Tungu, Robert Buduluba, Meshack Mashigala, Kashi Gacha, Shiwa Jasamila, Emmanuel Mwikabe na Makoye Kashinje.

Wengine ni Valerian Baleke, Yusuph Mbundi, Abdulmalik Hassan, Frank Alex, Mpanga Mpanga, Jimotoli Maduka, Elzeus Rwehumbiza, William Makune na Emmanuel Kibiriti.

Juzi, CCM ilifungua pazia kwa wanachama wake kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya chama kuteuliwa kuwania nafasi za udiwani, ubunge na uwakilishi.

# JPM amtumbua Makonda

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ameteua Aboubakar Kunenge kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuchukua nafasi ya Paul Makonda.

Uteuzi huo ulitangazwa jana jioni na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ikiwa ni saa chache baada ya Makonda kuchukua fomu ya kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuteuliwa kuwania ubunge wa Kigamboni jijini kupitia chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, ilieleza kuwa Rais Magufuli amefanya uteuzi wa viongozi wa mikoa 10 na wilaya nne.

Mbali na Kunenge ambaye kabla ya uteuzi wa jana alikuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mkoa wa Dar es Salaam, Rais Magufuli amemteua Joseph Mkirikiti kuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara.

Kabla ya uteuzi huo, Mkirikiti alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara na amechukua nafasi ya Alexander Mnyeti.

Katika taarifa yake hiyo, Msigwa pia alisema Rais amemteua Paul Makanza kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam. Kabla ya uteuzi huo, Makanza alikuwa Ofisa Mwandamizi wa Benki Kuu (BoT).

Msigwa alisema Rais amemteua Seleman Serera kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma na kabla ya uteuzi huo alikuwa Ofisa Mwandamizi wa CCM Makao Makuu na anachukua nafasi ya Deo Ndejembi.

Wengine walioteuliwa ni Sajini Taji (SSGT) Mayeka Simon ambaye anakwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya na kabla ya uteuzi huo, alikuwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi (JWTZ) na anachukua nafasi ya Marryprisca Makundi.

Rais Magufuli pia amemteua Kanali Patrick Songea kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara na kabla ya uteuzi huo alikuwa Ofisa Ulinzi wa JWTZ na anachukua nafasi ya Tumaini Magesa.

Pia, amemteua Alhaji Rajab Kundya kuwa Mkuu wa Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro na kabla ya uteuzi huo, alikuwa ofisa katika Ofisi ya CCM Makao Makuu na anachukua nafasi ya Kippi Warioba.

Rais pia amemteua Joseph Rwiza kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma na kabla ya uteuzi huo alikuwa Ofisa Mipango katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na anachukua nafasi ya Godfrey Kasekenya.

Vilevile, Rais amemteua Gharib Lingo kuwa Mkuu wa Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara na kabla ya uteuzi huo, alikuwa ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.

Frank Chonya ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi na kabla, alikuwa Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi na anachukua nafasi ya Andrea Chezue.

Wakati huo, Waziri ya Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika, kwa mamlaka aliyokasimiwa na Rais, amefanya uteuzi wa makatibu Tawala wa Wilaya.

Walioteuliwa ni Mashaka Mgeta kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni mkoani Tanga na anachukua nafasi ya Boniface Maiga aliyefariki dunia hivi karibuni.

Waziri Mkuchika amemteua Juveline Mwambi kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Tandahimba mkoani Mtwara na anachukua nafasi Benaya Kapinga.

Pia, amemteua Johari Athuman kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro na kabla ya uteuzi alikuwa ofisa katika Ofisi ya Rais na anachukua nafasi ya Aboubakar Asenga.

Waziri huyo pia amemteua Ayoub Perro kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi na kabla ya uteuzi huo, alikuwa ofisa katika Ofisi ya Upelelezi ya Polisi Mkoa wa Kigoma na anachukua nafasi ya Twaha Mpembenwe. Wateule wote wanatakiwa kuwapo Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma leo.

TEGEMEZA FINANCE COMPANY & COURT BROKER LIMITED
DEBT COLLECTION OFFICE MBEZI BEACH, S.L.P 77593, DAR ES SALAAM
tegemezacopanyltd@gmail.com Tel: 0762 443 118 /0719 187 677

TAREHE: 15/07/2020

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA NA NOTISI

TEGEMEZA & COURT BROKER LIMITED. KWA IDHINI TULIYOPEWA NA BANK YA NMB – MAKAO MAKUU KUTAKUWA NA UUZAJI WA NYUMBA NZURI ZA KISASA ZILIZOKUWA ZIMEWEKWA DHAMANA. BAADA YA MTEJA KUVUNJA MKATABA, ZINAENDA KUUZWA.

WATU WOTE MNAKARIBISHWA KWENYE MNADA HUU WA HADHARA.

TAARIFA ZA DHAMANA

| JINA LA MDAIWA | TAARIFA ZA NYUMBA | ENEO ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| JEROME JEROME TESHA | Licence No. TMK046935 MITA ZA MRABA 155 (sqm) | KEKO MAGURUMBASI MANISPAA YA TEMEKE | 8/8/2020 SIKU YA JUMAMOSI | SAA 4:30 ASUBUHI |
| FLORENCE MICHAEL TESHA | Licence No. TMK018589 MITA ZA MRABA 258 (sqm) | MBAGALA KWANYOKA MANISPAA YA TEMEKE | 8/8/2020 SIKU YA JUMAMOSI | SAA 4:30 ASUBUHI |

MASHARTI YA MNADA
1. Mali itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei iliyofikiwa ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14 toka muda ulipofanyika mnada.
3. Kama mnunuzi atashindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hatarudishiwa fedha alizo lipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi.
5. Wateja mnakaribishwa kukagua nyumba ndani ya muda wa kazi tu.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na ofisi ya Tegemeza Court Broker – Mbezi Beach, Dar es Salaam.
Simu: 0719 187 677

158126

HABARI KITAIFA

# Kizimbani tuhuma utakatishaji bil. 2/- za benki ya NMB

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI 20 wa jijini Dar es Salaam wakiwamo walinzi saba wa Kampuni ya Security Group of Africa (SGA), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo wizi na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni 2 mali ya benki ya NMB.

Washtakiwa hao ni Beda Mmali (51), John Selestine (45), Kaisi Nasibu (35), Edes Hyera (43), Osward Mselema (49), Olaph Mselema (35), Manjestus Mselema (44) na wenzao 14.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Luboroga.

Wakili wa Serikali, Faraja Nguka, alidai katika tarehe tofauti mwaka 2020 jijini Dar es Salaam, washtakiwa Mselema, Mwakuzi na wenzao sita walikula njama ya kuongoza genge la uhalifu ili kufanya kosa la wizi.

Ilidaiwa kwamba Juni 8, mwaka 2020 eneo la Mbezi Beach, jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote waliiba Sh. 2,082,000,000 mali ya Benki ya NMB.

Ilidaiwa kwamba katika tarehe hiyo, washtakiwa hao walitakatisha kiasi hicho cha fedha wakijua ni zao la kosa la wizi.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa, ambapo hakimu alisema ni Julai 28, mwaka huu.

Washtakiwa wote wamerudishwa rumande kwa kuwa mashtaka ya kutakatishaji fedha hayana dhamana.

# Corona kushusha uchumi wa dunia 5%

**Na Gwamaka Alipipi**

KUTOKANA na ugonjwa wa virusi vya corona kuathiri nchi nyingi duniani, imeelezwa kwamba uchumi wa dunia unatarajiwa kuporomoka kwa asilimia 4.9 mwaka huu.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mkutano wa kamati ya mawaziri wa fedha na uwekezaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Dk. Mpango ambaye aliwakilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu, alisema kwa mujibu wa taarifa ya matokeo ya kiuchumi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Juni, 2020, kuporomoka huko ni pungufu kwa asilimia 1.9.

"Machi 11, mwaka huu Shirika la Afya Duniani lilitangaza kuwa ugonjwa wa corona ni janga la dunia. Athari za ugonjwa huu zimegusa maeneo mbalimbali ya kiafya pamoja na kiuchumi," alisema Dk. Mpango.

Alisema mwaka jana, uchumi wa nchi nyingi wanachama wa SADC ulidorora kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo mvua kubwa zilizosababisha mafuriko na uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji, hivyo kuchelewesha utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo.

Alisema hali hiyo imesababisha kushuka kwa wastani wa ukuaji wa uchumi kutoka asilimia 2.8 kwa mwaka 2018 hadi asilimia 1.8 kwa mwaka 2019.

"Pamoja na changamoto hiyo ya wastani mdogo wa ukuaji wa uchumi tunajivunia kutambua kwamba nchi mbili wanachama zimeweza kufikia uchumi wa kati na juu, na hakuna nchi wanachama ambayo imeshuka daraja," alisema Dk. Mpango.

Dk. Mpango alisema Tanzania imetambuliwa kuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati kwa pato la mtu mmoja kuongezeka ma kufikia dola za Marekani 1,080 mwaka jana kutoka dola za Marekani 1,020 mwaka 2018.

Alisema Mauritius imepanda daraja na kuwa nchi yenye hadi ya kipato cha juu kilichotokana na kuongezeka kwa pato la mtu mmoja hadi kufikia dola la Marekani 12,740 kwa mwaka jana, kutoka dola za Marekani 12,050 mwaka 2018.

Aliongeza mafanikio hayo yanaleta chachu kwa nchi wanachama kujitathmini na kuangalia uwezekano wa kuleta maendeleo zaidi ya kiuchumi na kuchukua tahadhari ili uchumi zisiweze kushuka hadhi.

"Ili kukabiliana na changamoto hizo, nchi wanachama zinatakiwa kuendeleza jitihada za kuvutia uwekezaji na kuongeza tija katika uzalishaji," alisema Dk. Mpango.

Mapema Katibu Mtendaji wa SADC, Dk. Stegomena Taxi, alisema nchi wanachama wa jumuiya hiyo zinapaswa kuchukua hatua madhubuti katika kujiinua kiuchumi baada ya kuporomoka kulikosababishwa na ugonjwa wa corona.

Alisema nchi wanachama zinapaswa kuweka mikakati endelevu ya kuvutia wawakezaji pamoja na kuboresha mazingira ya biashara.



Watuhumiwa 20 wa wizi Benki ya NMB, wakiwamo walinzi saba wa Kampuni ya Security Group of Africa (SGA), wakiwa katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jana, kabla ya kusomewa mashtaka matatu ikiwamo wizi na utakatishaji zaidi ya Sh. bilioni 2 mali ya benki ya NMB. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtoto amwomba JPM msaada tiba

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MWANAFUNZI wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Gallapo, Babati mkoani Manyara, Hussein Mohamed (14) (pichani), ambaye anasumbuliwa na tatizo la moyo, amemwomba Rais John Magufuli na wadau wengine kumsadia kupata matibabu ili aendelee na masomo.

Ombi hilo alilitoa jana nyumbani kwao katika mtaa wa Sawee, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu maumivu anayoyapata.

Mtoto huyo alisema anajisikia vibaya sana na anashindwa kula na hata kuhema, hivyo anamwomba Rais na wadau wengine wamsaidie ili apate matibabu.

"Naomba Rais Magufuli anisaidie nipate matibabu ili niendelee kusoma nitimize ndoto yangu ya kuwa mwalimu niwafundishe wenzangu," alisema Mohamed.

Stella Jacob (38), ambaye ni mama wa mtoto huyo alisema mtoto wake alianza kuugua Septemba, mwaka jana.

Mama huyo alisema baada ya kuanza kuumwa alimpeleka Hospitali ya Mji wa Babati ya Mrara na akaambiwa ni malaria na alitumia dawa bila mafanikio.

Alisema alipoona bado kuna tatizo, alimrudisha hospitali hiyo na kuambiwa ana kifua kikuu ndipo alianza kutumia dawa.

Baada ya kutumia dawa ya kifua kikuu bila kupona, alisema baadaye kuna daktari mmoja alimpima akasema shida yake si kifua kikuu bali ana tatizo la moyo na akatakiwa kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara.

"Moyo wake unakuwa mkubwa umetanuka na tumbo linajaa maji mpaka anashindwa kula na kuhema. Nahangaika naye mno naomba msaada," alisema Jacob.

Alisema alipomfikisha Hospitali ya Rufani ya Mkoa, alipewa rufani ya kumpeleka Hospitali ya Benjamin Mkapa na gharama za matibabu yake ni Sh. milioni 8.4.

Mama huyo alisema hana uwezo kwa kuwa anaishi peke yake baada ya kutelekezwa na mume wake toka mwaka 2001 na kumwacha na watoto watatu. Kutokana na hali hiyo, alimwomba Rais Magufuli amsaidie ili mtoto wake atibiwe.

Naye Anna John, jirani yake na mama huyo alikiri mtoto huyo kuumwa na mpaka usiku huwa anamwamsha ili amsaidie kumpeleka duka la dawa ili akapate dawa ya kumtuliza.

Kwa upande wake, Martine Nade, jirani wa eneo hilo, alisema baada ya mama huyo kupewa rufani ya kwenda Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma, waliamua kuanza kuchangisha mchango mtaani na mpaka sasa wamekusanya Sh. 120,000.



Nade alisema wanapokutana na madaktari na wauguzi, wanawashauri wamuwahishe hospitalini kwa kuwa hali yake si nzuri.

Kwa atakayeguswa na tatizo hili mawasiliano ya mama ni **0684613865.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusichezee uteuzi tuibue wawajibikaji

**MINONG'ONO** kuwa ni nani atakuwa mgombea wa urais Bara na Zanzibar imekwisha sasa na kinachoendelea ni kukamilisha uteuzi wa wagombea wa udiwani na ubunge kutoka vyama vilivyosajiliwa vitakavyoshiriki uchaguzi mkuu ili kuanza mchakato wa kampeni.

Kinachotazamiwa kuanzia sasa ni kuona majina ya viongozi watarajiwa waadilifu na wawajibikaji wakiteuliwa na vyama vyao kugombea ubunge na udiwani ili kufanya kazi si za chama wala matamanio yao bali za kusaidia kuleta maendeleo kwa vijana, wazee, kinamama na wanyonge ili Tanzania isonge mbele.

Tunaona kuwa kazi aliyoifanya Rais John Magufuli kwa miaka mitano inaonyesha kuwa Watanzania wanatarajia kuona mabadiliko siyo kubabaisha, iwe miradi ya maendeleo, utendaji na kwa ujumla kufanyakazi kwa ajili ya wanyonge.

Tunaamini wapigakura wana hamu ya kuona wawakilishi wao na wabunge ambao wataunda baraza la mawaziri lenye mawaziri wanaoshughulikia matatizo ya watu na wanaojibu hoja za wananchi ambao tangu mwanzo wameonyesha nia ya kuona ukweli wa msimamo wa 'Magufuli for Changes' ambayo imeifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati.

Wapigakura wamechoka kuona magari ya bei mbaya au mashangingi ama V8 ambayo viti vyake vimefunikwa na vitambaa vyeupe yakiwabeba wabunge wao ambao hawasaidii kubadili maisha yao wala hawawatembelei kujua dhahama zao badala yake wanakuja kipindi hiki cha uchaguzi..

Tuna imani kuwa watakaoteuliwa ni wale watakaoishauri serikali namna bora ya kutatua matatizo ya ukosefu wa ajira, huduma bora za kijamii, lishebora na mengine yanayowakwamisha kuondokana na umaskini.

Wapiga kura wanatarajia kupata wabunge na madiwani watakaoishauri serikali na halmashauri zao namna bora ya kuhakikisha kuwa wamachinga wanaosota kwenye miji mbalimbali wakiuza bidhaa kandokando au ndani ya barabara kuu wanapata viwanja vya kufanyia biashara zao vyenye usalama na miundombinu bora.

Aidha, wanatarajiwa wabunge na madiwani wanaofikiria kuandaa na kushauri serikali na halmshauri mikakati na mbinu za kuboresha maisha ya wananchi, kuondoa uchafu mitaani na kuhakikisha watu hawafi kwa mafuriko kisa wanaishi mabondeni.Vijijini wanawake wanatarajia kumalizika kero ya kupeleka ndoo za maji, mafuta ya taa ili kuwashia taa na kuni za kujipikia vyakula hasa wajawazito wenye uhitaji wa wataalaumu wanaolazimika kukaa hospitalinni.

Licha ya serikali kugharamia elimu bado mabinti hawasomi wanapata mimba, kuolewa utotoni na changamoto kubwa ni kuendeleza mila na desturi zinazowaumiza wanawake na watoto.Viongozi watarajiwa wanatarajiwa kuisaidia serikali kuondokana na changamoto hizo na kuweka mazingira sawa ya kijinsia ili kila raia awe na haki ya kupata na kufurahia maisha bora.

Tunaamini viongozi wanaotarajiwa kuchaguliwa wanategemewa kuwa waadilifu na wanaoendana na kasi ya 'hapa kazi tu' na kuhudumia wananchi.

Ni wale walio mstari wa mbele kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na kuondoa usumbufu kwa wananchi ili kuzifikisha huduma za kijamii na kupunguza malalamiko ya raia waliowachagua pamoja na umaskini.

Tunaona kuwa awamu hii matatizo ya wananchi yamepunguzwa kwa mfano ukiingia hospitali za umma nyingi zinaelezwa kuwa zina dawa na kinachosisitizwa sasa ni wananchi kuwa na bima ya afya ili kujigharamia matibabu.

Tunahimiza kuwa madiwani na wabunge watarajiwa wanatakiwa wawajibike wawe wasikivu na wanaofuatilia matatizo ya wananchi kama mashine hospitalini mfano x-ray, ultrasound na uwapo wa huduma muhimu kwa umma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Afya pia inategemea maji, wanajamii tuvilinde vyanzo

**MAJI** ni muhimu kwa viumbe vyote duniani. Serikali kupitia kampeni yake inasema 'Maji ni Uhai.' Maana yake ni kwamba, bila ya maji, hakuna uhai unaofanyika.

Pia, ni hitaji la kiafya na maendeleo ya kiuchumi na kijamii, hivyo inakuwa muhimu kutunza na kulinda vyanzo vyake.

Vilevile, upatikanaji majisafi na salama kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na usafi wa mazingira, ni sahihi mno katika kulinda afya za umma.

Hiyo ni kwa sababu, matumizi ya maji machafu yanachangia milipuko na kuenea magonjwa. Hapo panatajwa maradhi kama kuhara na kipindupindu.

Hapo ndio sababu ya kuwapo haja ya kuharakisha uwiano wa mgawanyo wa maji, kati ya sehemu moja na nyingine ndani ya jamii.

Juhudi zimefanyika kwa ajili ya kuhakikisha huduma hiyo inatosha nchini, lakini bado yapo baadhi ya maeneo nchini, upatikanaji maji ni changamoto kubwa kwao.

Kuna baadhi ya maeneo ambayo huduma hiyo inapatikana, kukiwapo changamoto zake. Watu hawalindi mindombinu ya maji na hawazingatii usafi wa mazingira yao, kwa ajili ya afya kwa ujumla.

Suala la kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji, ili kutoa huduma endelevu katika maeneo ya vyanzo vyake kwa jamii ya maeneo husika, ni jambo la msingi.

Mahali pa aina hiyo panapoachwa, matokeo yake ni hatari. Uimarishaji na uhifadhi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji au katika visima vya maji, kunaweza kuboresha afya ya jamii kwa kuzingatia usafi wa mazingira na elimu ya afya.

Kwa ujumla, afya ya jamii inalindwa na jamii yenyewe kuhamasishana kuhusu matumizi bora ya vyoo, kutotupwa takataka ovyo na umuhimu wa upatikanaji huduma ya maji ya kutosha na salama. Hivyo, ni vyema sasa jamii ikatambua umuhimu wa kulinda vyanzo, visima na mabomba ya maji yaliyopo kwa ajili ya usalama wa afya na mengine ya maendeleo.

Pamoja na jitihada za kiserikali kuendeleza huduma za maji kuanzia miaka ya 1970, ni jambo linaweza zikakwamishwa na baadhi ya wasiojua umuhimu wa kulinda vyanzo hivyo, visima na mabomba ya maji.

Lengo la Sera ya Maji ya mwaka 1991, lilikuwa ni kufikia mwaka 2002, serikali iwe imewapatia wananchi wote majisafi na salama katika umbali usiozidi mita 400. Hata hivyo, bado haijatimia.

Jambo muhimu zaidi ni pale huduma za maji zilizopo zikalindwa, badala ya wananchi kujiweka kando wakiamini siyo jukumu lao kulinda huduma hiyo kwenye maeneo yao.

Katika bajeti iliyoko sasa, wizara husika imetenga Sh. 733,284,075,000 kuboresha huduma za maji nchini, hivyo fedha hizo zitakapofikishwa katika huduma, jamii iwe tayari kulinda miundombinu ya maji.

Upatikanaji maji salama katika jamii, ni muhimu kwa ajili ya kupambana na umaskini na matatizo ya afya, kwani watu maskini ambao wengi wao wanaishi vijijini, wana nafasi finyu ya kupata huduma hiyo.

Kama nilivyoeleza awali, baadhi yao wanapopata huduma hiyo huwa ni wazembe kuitunza, hali ambayo kwa namna moja au nyingine, inachangia kuendelea kuwapo huduma duni ya maji.

Ikumbukwe kwamba magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya maji yanaweza kupatikana zaidi katika sehemu ambayo watu wanatumia maji yasiyo salama, wakati mwingine kwa kuchafuliwa wanajamii yenyewe.

Hivyo, umuhimu wa kulinda na kutunza vyanzo, visima na mabomba ya maji uko palepale kwa afya ya jamii husika na siyo kusubiri kutoka sehemu nyingine kuja kusimamia ulinzi.

Majisafi na salama ni yapi? Ni yale yasiyokuwa na uchafu na yako sahihi kiafya na kinyume chake ndiyo yasiyofaa kwa matumizi na hata mtumiaji kuishia kuhara na maradhi mengine kama kipindupindu.

Kuna njia mbalimbali za usafi katika vyanzo vya maji ikiwamo, kutumia visima vyenye mifuniko na kuhakikisha vinafunikwa baada ya kuteka maji, kunasaidia kuepuka taka kuingia visimani.

Ni bahati mbaya, kuna maeneo ambayo jamii haijaweka ulinzi katika visima vyao na hata inavifanya visiwe salama. Wapo wanaoiba mifuniko kwenda kuviuza kama chuma chakavu.

Hivyo ni tabia iliyozuka katika siku za karibuni, baada ya kuzuka tabia hiyo ambayo iko dhahiri inaweza kumalizwa kwa jamii yenyewe kutambua na kuthamini huduma ya maji, inapopewa ulinzi stahiki.

# HABARI PICHANI



Wajumbe wa Mkutano Mkuu maalumu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Singida Mjini, wakimpongeza Rehema James (katikati), baada ya kuchaguliwa na mkutano huo kugombea nafasi ya ubunge mjini humo, juzi. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**



Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), Geofrey Mwambe (kushoto), akipokea fomu ya kuomba kuteuliwa kuwa mgombea wa ubunge wa Jimbo la Masasi kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), mjini Masasi, mkoani Mtwara jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**



Waziri wa Uwekezaji, Angellah Kairuki (kulia), akichukua fomu ya kuomba kuteuliwa kuwa mgombea ubunge Jimbo la Same Magharibi, kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kutoka kwa Katibu wa chama hicho, Wilaya ya Same, Victoria Mahembe, juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**



Kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Emanuel Kamara (kulia), akipokea fomu ya kuomba kuteuliwa kuwa mgombea ubunge Jimbo la Dodoma Mjini kutoka kwa Katibu Msaidizi wa CCM Wilaya ya Dodoma, Saidi Ngomboi, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Mtoto wa Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, Samweli John Malecela (kulia), akipokea fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge Jimbo la Chilonwa, kutoka kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Chamwino, Evelyin Jordan, wilayani humo, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Mwakilishi wa jimbo la Tunguu anaetetea jimbo lake, Simai Mohamed Said (katikati) akipokea fomu ya kugombea uwakilishi wa jimbo hilo kutoka kwa Katibu wa CCM wilaya ya Kati, mkoa wa Kusini Unguja, Omar Justus (kulia) katika hafla iliyofanyika kwenye ofisi ya CCM Dunga jana. Kushoto ni Katibu Mwenyezi wa CCM wa wilaya hiyo, Abdalla Maru. **PICHA: MARTIN KABEMBA**



Raia wa China, Hu Kai, akisindikizwa na askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 27 kwa kosa la kuisababishia hasara serikali zaidi ya shilingi bilioni moja. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wachina, Mtanzania jela kukwepa kodi

**Na Hellen Mwango**

RAIA wawili wa China na Mtanzania mmoja wamehukumiwa kwenda jela miaka 30, baada ya kupatikana na hatia ya makosa matano kati ya sita ikiwamo kukwepa kodi na kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 1.776.

Kadhalika, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaifi, imeamuru washtakiwa hao wakimaliza kutumikia kifungo kulipa fidia ya fedha hizo walizosababisha hasara.

Washtakiwa ni raia wa China na wafanyabiashara Gu Kai (49) na Jason Wei (30) na Mtanzania Jovin James (28), mkazi wa Tabata.

Hata hivyo, Mahakama hiyo imemuachia huru Leornad Assey (26), baada ya upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yake.

Hakimu Shaidi alisema upande wa Jamhuri kupitia mashahidi tisa umethibitisha makosa bila kuacha shaka kuwa washtakiwa hao watatu wametenda makosa hayo matano, na amewaachia huru katika kosa moja la kula njama.

Hakimu Shaidi amedai, katika shtaka la kughushi washtakiwa watatumikia kifungo cha miaka saba na katika kosa la kutoa nyaraka za uongo wamehukumiwa miaka saba, huku shtaka la kujipatia usajili kwa udanganyifu miaka miwili, kusababisha hasara miaka saba pamoja na kosa la kukwepa kodi.

Hata hivyo, adhabu zote nitaenda pamoja hivyo, watakaa gerezani kwa miaka saba

Haqta hivyo, wakati hukumu hiyo inasomwa, mshtakiwa Wei hakuwapo mahakamani baada ya kuruka dhamana na mahakama imeamuru atafutwe ili kutumikia kifungo chake.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wote wanadaiwa mwaka 2014 jijini Dar es Salaam, walikula njama ya kutenda kosa ambapo wanadaiwa Oktoba 21, 2014 Dar es Salaam walighushi fomu ya taarifa za mteja wakionyesha kwamba kampuni ya Calcare International Company Ltd imeomba mashine ya EFD kwa Compulynx Tanzania Ltd wakati siyo kweli.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa siku na mahali hapo mshtakiwa Jovina na Gu Kai waliwasilisha kwa Compulynx T Ltd fomu ya taarifa ya mteja wakidai kampuni ya Calcare iliomba mashine ya EFD huku wakijua siyo kweli.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa, siku na mahali hapo washtakiwa kwa nia ya kudanganya walijipatia usajili wa EFD mashine kutoka TRA kwa kujidai kwamba mashine hiyo ingetumiwa na Calcare, huku wakijua siyo kweli.

Iliendelea kudaiwa kati ya Oktoba 21, 2014 na Machi 30, 2016 jijini Dar es Salaam, washtakiwa Leornad na Jason wakiwa watu wanaojihusisha na uendeshaji wa shughuli za kampuni za Tifo Global Mart (Tanzania) na Lotay Steel ( Tanzania) Ltd kwa nia ya kudanganya, walitumia EFD mashine iliyosajiliwa na Calcare na kukwepa kodi ya Sh. 1,776,693,465

Katika shtaka la mwisho, inadaiwa katika kipindi hicho hicho, washtakiwa wote kupitia vitendo vyao waliisababishia TRA hasara ya Sh. 1,776,693,465 kwa kusajili EFD mashine na baadae kuitumia kutoa risiti feki kufuatia mauzo yaliyofanywa na kampuni ya Tifo na Lotay

SGA SECURITY

**Tunasherekea Maisha ya Mwasisi Wetu**

Bodi, Utawala na wafanyakazi wa SGA Security pamoja na familia, tunasikitika kutangaza kifo cha mwanzilishi wa kampuni ya SGA Security, Mzee Philemon Nathaniel Mgaya, kilichotokea mnamo tarehe 14 July,2020, Dar es salaam. Mzee Mgaya alikuwa mstaafu Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP). Walianzisha SGA Security na mwenzake (wakati huo ilijulikana kama Group Four Security) mnamo mwaka 1984, ikiwa kampuni ya kwanza kwenye sekta binafsi ya ulinzi hapa Tanzania. Hivyo ameacha pengo kubwa, sio kwa familia tu, bali hata kwa wafanyakazi, sekta binafsi ya ulinzi na Tanzania kwa ujumla. Mzee Mgaya alijaliwa kuishi miaka zaidi ya 90 na aligusa na kuboresha maisha ya wengi. Anapopumzika, anaacha familia yake ya karibu na familia ya wafanyakazi 5,800 wanaomfanyia kazi SGA hapa Tanzania.




***Mzee Philemon Nathaniel Mgaya***

**Kuadhimisha maisha yake, ibada ya mazishi imepangwa kufanyika Azania Front Lutheran Church, Dar es Salaam siku ya Jumamosi tarehe 18/07/2020 kuanzia saa tano asubuhi. Atazikwa nyumbani kwake Usangi, mkoa wa Kilimanjaro, siku ya Jumatatu tarehe 20/07/2020.**

www.SGAsecurity.com

158139

# Kampuni ya Twiga yazipiga jeki h'shauri

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya Twiga Minerals Corperation Limited, inayomiliki migodi miwili ya dhahabu ya Buzwagi na Bulyanhulu Wilayani Kahama Mkoani Shinyanga, imekabidhi hundi ya Sh. billioni 1.5 kwa Halmashauri mbili Wilayani Kahama.

Malipo hayo ni moja ya ushuru wa huduma kwa kipindi cha Januari, 2020 hadi Juni , mgodi wa Buzwagi ukilipa Sh.bilioni 1.1 kwa Halmashauri ya mji wa Kahama, huku mgodi wa Bulyanhulu ukilipa Sh. milioni 376 kwa Halmashauri ya Msalala.

Akikabidhi hundi hiyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, Meneja wa migodi miwili ya Bulyanhulu na Buzwagi, Benedict Busunzu, alisema malipo hayo yanafanyika ikiwa ni kutekeleza hitaji la kisheria, lakini pia ikiwa ni sehemu ya mikataba ya makubaliano kati ya migodi hiyo na Halmashauri mbili husika.

Busunzu alisema malipo hayo yanalenga kutatua kero na kuboresha huduma mbalimbali katika sekta ya afya, elimu, maji katika jamii zinazozunguka migodi hiyo na ziweze kunufaika na uwapo wa migodi hiyo katika maeneo yao.Alisema mgodi huo umekuwa ukitoa fursa endelevu za kiuchumi na maendeleo kwa jamii katika sekta za kilimo, ufugaji ikiwa ni kuinua uchumi wa wilaya na kuboresha maisha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

"Tunafarijika sana kwa ushirikiano ambao tumekuwa tukiupokea kutoka kwa wananchi ambao walikuwa wakiibua miradi mbalimbali na serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo unasaidia kufanikisha juhudi zetu za kujenga jamii endelevu," alisema Busunzu.

Akipokea hundi hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Macha alisema kazi zinazofanywa na migodi hiyo ni moja ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuzitaka Halmashauri husika kuzitumia fedha hizo kwa miradi iliyokusudiwa ambayo italeta tija na mabadiliko kwa wananchi, kwa kutatua kero na kuboresha huduma za jamii.

Macha alisema wananchi kwa sasa wanahitaji maendeleo hasa kwa kutumia wawekezaji waliopo na kuongeza kuwa fedha zilizotolewa na wawekezaji hao thamani yake iendane na miradi itakayokuwa imetekelezwa na halmashauri husika.

HABARI KITAIFA



Mshtakiwa mkazi wa Kijiji cha Kalya, Wilaya ya Uvinza, Winston Samigwa (69), akiwa chini ya ulinzi mkali wa polisi katika Mahakama ya Wilaya ya Kigoma jana, baada ya kuhukumiwa miaka 20 jela kwa makosa matatu ya kukutwa na ngozi moja ya chui na jino la ngiri vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 8 pamoja na mitengo 20 ya kuwindia wanyama pori bila kuwa na kibali. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Ngozi ya chui, jino la ngiri vyampeleka jela miaka 20

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Kalya, Wilaya ya Uvinza, Winston Samigwa (69), kutumikia kifungo cha miaka 20 jela kwa makosa matatu ya kukutwa na ngozi moja ya chui na jino moja la ngiri.

Nyara hizo zina thamani ya Sh. milioni 8 pamoja na mitengo 20 ya kuwindia wanyamapori bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu wa Mahakama hiyo, Katoki Mwakitalu, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa hayo yote pasi shaka yoyote.

Hakimu Mwakitalu alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Raymond Kimbe, ulipeleka mashahidi watano na vielelezo vinne ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alikamatwa na ngozi moja ya chui, jino moja la ngiri pamoja na mitego 20 ya kuwindia wanyama pori kinyume cha sheria.

Aidha, alisema Novemba 7, mwaka 2018 askari wa wanyamapori wa Hifadhi ya Taifa ya Mahale walipata taarifa kutoka kwa wasiri wao kwamba mshtakiwa huyo anamiliki ngozi ya chui, na kuwa baada ya kupata taarifa hizo walikwenda kituo cha Polisi Kalya Wilaya ya Uvinza kwa ajili ya kuongeza nguvu.

Alisema walipofika kituo cha polisi katika Kijiji cha Kalya waliondoka na mkuu wa kituo hicho hadi nyumbani kwa mshtakiwa huyo, ambao walimkatamata na kumtaka awaonyeshe ngozi moja ya chui na jino moja la ngiri, ndipo mshtakiwa huyo alipochukua jembe na kuchimba chini ya jiko la nyumba yake na alipofukuwa alitoa mfuko wa sandarusi ndani yake kulikuwa na ngozi moja ya chui, jino moja la ngiri na mitego 20 ya kuwindia wanyamapori.

Aidha, alisema baada ya zoezi hilo walimkamata mshtakiwa na vitu hivyo na kumpeleka katika Kituo cha Polisi Kati Manispaa ya Kigoma/Ujiji na baada ya mahojiano walimpeleka mahakamani.

Hakimu Mwakitalu alisema upande wa mashtaka umethibitisha makosa yote matatu pasipokuacha shaka yoyote, hivyo mshtakiwa umetiwa hatiani kwa makosa yote aliyoshtakiwa nayo.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Kimbe alidai Novemba 8, mwaka 2018 askari polisi na askari wa Hifadhi ya Taifa ya Mahale walimkamata mshtakiwa huyo nyumbani kwake Kijiji cha Kalya Wilaya ya Uvinza Mkoa wa Kigoma akiwa na nyara hizo za serikali.

# Vigogo wa CHADEMA Ubungo watua ACT

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimepata pigo baada ya baadhi ya wanachama wake akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wake Wilaya ya Ubungo, Renatus Pamba, kuhamia Chama cha ACT-Wazalendo.

Imedaiwa kuwa, chanzo cha wanachama hao kukihama chama hicho kikuu cha upinzani nchini, ni kile wanachoona ukiukwaji wa Katiba ya chama hicho baada ya kuwavua uongozi.

Akizungumza jana jijini na waandishi wa habari kwa niaba ya wanachama wenzake waliohama, Pamba alidai uongozi wa Kanda ya Pwani haukufuata Katiba ya chama ulipotangaza kuwavua uongozi bila kuwapa nafasi ya kuwasikiliza.

Alidai hatua hiyo imelenga kumpendelea mmoja wa watia nia ya kuwania ubunge katika Jimbo la Ubungo ambaye hata hivyo, hakumtaja.

"Mimi Renatus Pamba, nilitia nia kugombea ubunge wa Ubungo na baada ya kuonyesha nia hiyo, figisu zikaanza za kuvunjwa uongozi niliokuwa ninauongoza mimi Kamati ya Utendaji ya Jimbo," alidai.

Aliyekuwa Katibu Mwenezi wa Jimbo hilo, Alex Sebastian, alidai kuwa kitendo cha kuvunjwa kwa uongozi wa jimbo hilo saa saba za usiku na uchaguzi wa viongozi hao kufanyika asubuhi, ni ishara ya wazi ya kutokufutwa kwa misingi ya kidemokrasia ya chama hicho.

Alisema hatua hiyo ilichukuliwa kwa malengo maalumu ya mtia nia mmoja wapo wa ubunge katika jimbo hilo kuweka safu yake. "Tunatambua kuwa uongozi wa kanda unaweza kuwa na mamlaka zote za kuvunja uongozi, lakini ni lazima kufuata katiba," alidai Sebastian.

"Makamu Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani na Katibu wa Kanda, Ndugu Hemed Ally pengine hawaifahamu vizuri Katiba," aliongeza.

Baadhi ya watia nia katika Jimbo la Ubungo walioomba ridhaa ya chama hicho kuwania ubunge ni pamoja na aliyekuwa Mbunge wake, Saed Kubenea na aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Jacob.

## NMB yashinda tuzo ya umahiri

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB kwa mara ya nane mfululizo imeibuka benki bora Tanzania kwa mwaka 2020 katika tuzo zinazotolewa na jarida la kimataifa la Euromoney. Imepata ushindi huo baada ya kuzishinda benki nyingine 40 nchini. Hii ni tuzo kubwa inayotolewa na jarida la kimataifa la masuala ya fedha linaloongoza duniani la jijini London - Uingereza. Tuzo hiyo hutolewa kwa kuzingatia vigezo kadhaa kwa benki zilizopendekezwa ukiwamo ufanisi wa hesabu za fedha na utendaji kwa ujumla, mkakati wa huduma za kidijitali, huduma jumuishi za fedha, usalama wa huduma za kimtandao na wajibu wa benki kwa jamii inayoihudumia.

Vigezo vingine ni mtaji wa benki, mapato yatokanayo na biashara ya hisa, mapato yatokanayo na mali za kampuni, pato litokanalo na riba, uwiano wa fedha na gharama za uendeshaji, kiwango cha amana za wateja, kiwango cha mikopo katika soko, uwiano kati ya mikopo na amana za wateja, uwiano wa mikopo chechefu, uwiano wa hasara itokanayo na mikopo chechefu.

Akizungumza kabla ya kukabidhiwa tuzo hii, Mwenyekiti wa Bodi ya NMB, Dk. Edwin Mhede, alisema baada ya Tanzania kufikia uchumi wa kati, Benki ya NMB inaahidi kuendelea kutoa ushirikiano wa karibu ili kuchangia zaidi katika ukuaji wa Uchumi kwenda katika hatua ya juu zaidi. "Benki ya NMB itaendelea kujipanga na kutoa ushirikiano wa Karibu kwa serikali katika juhudi za kujenga uchumi imara zaidi," alisema. Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema: "Leo hii tunajulikana kama benki imara zaidi, yenye huduma za ubunifu wa kiteknolojia." "Lengo la benki ya NMB ni kuchangia zaidi kwenye uchumi wa Tanzania. Tumejitoa kuwa zaidi ya taasisi ya huduma ya fedha - tunachochea mabadiliko ya kiuchumi katika nchi yetu na kuboresha maisha ya Watanzania wenzetu kwa kutoa huduma zinazowafaa na kukidhi mahitaji na mipango yao nchi nzima," aliongeza Zaipuna na kusisitiza kwamba kushinda tuzo hiyo kwa mwaka wa nane mfululizo kunadhihirisha kujitoa kwa Benki ya NMB kwa wateja wake na Tanzania kwa ujumla.

Vilevile, alisema: "Tunatumia teknolojia bora zaidi kutoa huduma za kibenki kidijitali, ubunifu wa huduma na bidhaa zetu, upanuzi wa mtandao wa matawi na mawakala kusogeza huduma jirani zaidi na wananchi kuwapa thamani ya fedha na kuboresha maisha yao." Tuzo ya umahiri ya Euromoney inathibitisha uwekezaji wa benki kwenye teknolojia za kidijitali ulivyoimarisha uwezo wake wa kutoa huduma za kibunifu sokoni. Taarifa za fedha ya mwaka 2019 inaonyesha kuwa benki yetu ilipata faida ya Sh. bilioni 142 baada ya kodi ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 46 ikiongezeka kutoka Sh. bilioni 98 iliyopatikana mwaka uliotangulia na kuendelea kuwa benki yenye faida kubwa zaidi nchini kwa zaidi ya muongo mmoja sasa. Akizungumzia mchakato wa kumpata mshindi wa tuzo ya benki bora nchini, mhariri wa Jarida la Euromoney, Clive Horwood alisema: "Tunaendelea kuzitambua taasisi bora zaidi katika kila nchi ambazo zinazotoa huduma za fedha. Kwa kila mwaka, ukubwa ni muhimu lakini sio kigezo muhimu zaidi."

# Waganga tiba asili, mbadala wapewa siku 21

**Na Welingtone Masele,** KALIUA

SERIKALI wilayani Kaliua mkoani Tabora imetoa siku 21 kwa waganga wote wanaotoa huduma za tiba asili na tiba mbadala wilayani humo kuwa na vibali maalumu vitakavyowatambulisha mahali popote watakapokuwa.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Utamaduni wa Halmashauri ya Wilaya hiyo alipokuwa akizungumza na kwa niaba ya mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya hiyo na mamia ya wananchi waliohudhuria hafla ya kuwaaga waganga 24 waliohitimu mafunzo ya utoaji tiba asilia na tiba mbadala iliyofanyika katika Kijiji cha Kagera, Kata ya Kashishi.

Alisema baadhi ya waganga wanaotoa huduma hizo wamekuwa wakifanya shughuli hizo kiujanja ujanja pasipo kufuata taratibu, hali ambayo imekuwa ikipelekea kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Alisisitiza kuwa ili kuepuka usumbufu wanaopata sasa, kila mmoja anapaswa kukata kibali kitakachomruhusu kufanya shughuli hizo kwa uhuru na mahali popote pale nchini badala ya kujificha.

Kapela alibainisha kuwa serikali inatambua mchango wa waganga wa tiba asilia na tiba mbadala katika kuhudumia wananchi, ndiyo maana iliweka utaratibu mzuri wa kuwasajili kwa lengo la kutambulika na kutobughudhiwa.

Aliongeza kuwa serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilishaweka utaratibu pia wa kusajili kwenye Baraza la Tiba Asilia na Tiba Mbadala ili wapeane uzoefu wa kazi zao na kutatua matatizo yao. "Nawapongeza wote mliopata mafunzo haya, katoeni huduma isiyo na ubabaishaji wala visingizio vya aina yoyote, msijihusishe na ushirikina wala vitendo vya upigaji ramli chonganishi, atakayeenda kinyume na haya atakamatwa," alisema.

Msimamizi Mkuu wa Mafunzo hayo, Kulwa Buganga Ndomelo, alisema hadi sasa jumla ya watu 71 kutoka mikoa ya Tabora, Kigoma, Shinyanga, Geita, Katavi, Mwanza, Rukwa na Simiyu wameshahitimu mafunzo hayo tangu aanze kutoa huduma hiyo mwaka 2013.

Alisema kuwa wanafunzi hufundishwa namna ya kutumia miti, mimea na udongo katika kutoa huduma za tiba asilia na tiba mbadala kwa jamii na kwamba tiba hiyo haihusiani na ushirikina wala ramli chonganishi.

Aidha, aliongeza kuwa mafunzo hayo yanatolewa bure na yanafundishwa kwa miezi sita.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede (katikati), akipongezana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Ruth Zaipuna, baada ya benki hiyo kupata tuzo ya Euro money ya jijini London, iliyoitaja NMB kama Benki Bora nchini Tanzania, katika halfa iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Benki ya NMB imetwaa tuzo hiyo kwa mara ya nane mfululizo tangu mwaka 2013. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi. **PICHA: NMB**

# Watumiaji umeme kuanza kulipia kiasi wanachotumia

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo nchini (WMA), unatarajia kuanza kupima mita za umeme kuanzia Oktoba mwaka huu, ili kuwawezesha watumiaji wa nishati hiyo kuwa na uhakika wa kiasi wanachotumia na wanacholipia.

Hayo yalisemwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Dk. Ludovick Manege, wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe.

Prof. Shemdoe alitembelea kituo cha kupima kiasi cha mafuta kwenye matangi ya malori na mita za maji cha WMA kilichoko Misugusugu, mkoa wa Pwani kuangalia utendaji kazi wa kituo hicho.

Dk. Manege alisema mkandarasi wa kuleta mtambo huo ambaye ni Mjerumani amemhakikishia kuwa mtambo huo utakuwa umefika na kusimikwa Oktoba, mwaka huu.

Alisema mtambo huo utagharimu Sh. milioni 600, na kwamba kwa sasa WMA inashughulikia jengo ambalo mtambo huo utawekwa utakapowasili ili uweze kuanza kazi haraka.

"Tunataka uchaguzi ukimalizika tu basi mtambo uwe umeshaanza kufanyakazi kwasababu tunataka kuhakikisha mtumiaji wa mita hizo anapata kiwango sahihi cha umeme na analipa kiwango sahihi bila kupunjwa," alisema.

Aidha, alisema mbali na kupima mita za maji na umeme wako mbioni kuanza kupima ujazo sahihi wa gesi lengo likiwa kuhakikisha wananchi wanapata ujazo unaostahili.

"Tumeona bajeti kubwa ya utekelezaji wa miradi ya usambazaji wa maji na mradi wa umeme wa Rufiji na nchi inajielekeza kwenye utekelezaji wa miradi ya gesi sasa sisi WMA lazima tujipange kuhakikisha wananchi wanapata maji, umeme na gesi kwa vipimo sahihi na kupila viwango sahihi," alisema.

Kwa upande wake, Prof. Shemdoe alisema amejionea namna mita za maji zinavyopimwa kuwahakikishia vipimo sahihi wananchi na malori ya mafuta ili kupata vipimo sahihi.

Alisema kazi hizo hazifanyiki bure kwani kwa kila mita serikali imekuwa ikipata 10,000 hivyo kila mita inayoingia nchini inapaswa kupitia WMA kwa ajili ya kukaguliwa kama iko sawa.

"Hawa wameanza ununuzi wa mtambo wa kupima mita za umeme sasa naomba mchakato huo ufanyike haraka mtambo uje ili wenzetu wa TANESCO nao walete mita zao zihakikiwe hapa," alisema Shemdoe.

Aliagiza pia WMA ianze mchakato wa kuagiza mtambo kwa ajili ya kupima mita za gesi zinazotumika kwenye viwanda na maeneo mengine ili wananchi walipe kile wanachotumia.

"WMA mhakikishe mnashirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kuhakikisha mchakato wa kuleta mtambo wa gesi unafanyika ili kuhakikisha wananchi wanalipa kile wanachotumia," alisema Prof. Shemdoe.

## Benki ya Stanbic yataja sababu za mafanikio yake

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya Stanbic imesema safari ya ukuaji na mafanikio ambayo imeyapata kwa kiwango kikubwa yametokana na imani ya wateja wake.

Mkurugenzi Mkuu wa Benki hiyo, Kevin Wingfield, alisema imani hiyo ya wateja kwa benki hiyo imesaidia kuleta mabadiliko na motisha na kwao katika kuendelea kuboresha zaidi huduma zake.

"Benki ya Stanbic inaamini kuwa ndoto ni chachu ya maendeleo. Hivyo ni lazima sisi na wateja wetu tuwe tayari kuchukua hatua mpya kufanikisha ndoto hizo," alisema Wingfield.

"Wateja hutafuta mtoa huduma ambaye anawaamini na anawahamasisha. Wanahitaji benki inayowasaidia kufikia malengo yao binafsi na kibiashara na ambayo itawathamini katika kila jambo na ndiyo maana benki yetu tumeangalia mambo ambayo yana manufaa kwa wateja wetu na tukayafanyia kazi," alisema Wingfield.

"Mwelekeo huu ni kwa ajili ya kuhamasisha imani yetu juu ya Tanzania ya kesho, huku tukionyesha ubunifu wa suluhu ambazo zinalenga kutoa huduma fanisi kwa wateja wetu na pia kuhakikisha wateja wetu wanapata suluhu hususani katika kipindi hiki chenye changamoto ya ugonjwa wa COVID-19."

Alisema Aprili mwaka huu, benki hiyo ilitoa ahueni ya ulipaji wa mikopo kwa muda wa miezi mitatu hadi sita kwa wateja wake ambao walishindwa kutimiza wajibu huo kutokana na madhara ya kibiashara yaliyotokana na mlipuko wa ugonjwa huo.

Pia, alisema ilianzisha shindano la ujasiriamali ambalo lililenga kutoa zawadi ya Sh. milioni 50 kwa biashara zilizoonekana kuwa bora zaidi ikiwa kwa lengo la kusaidia wateja kustahimili athari za COVID-19.

"Zaidi ya hayo, benki ilizindua Africa China Agency Proposition ambayo inasaidia kampuni kufanikisha shughuli zao za kibiashara na China, lakini ni wakati wa kuwa na simulizi zenye matumaini, imani na mtazamo chanya," alisema Wingfield.

ama

ALHAMISI JULAI 16, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Mapishi ya kuni yanavyowaua macho kinamama wa Z'bar**



Ukurasa 13

Kituo kinacholea wenye mazingira magumu 'wastaafu' wao waungana



Ukurasa 14

**Dk. Leyna: Madini joto shida kubwa katika lishe ya umma**

AFYA

# Mkasa mimba ya kubakwa aliyojiunga nayo sekondari

## • Ndoto ualimu 'baibai' Likizo Corona

**Na Neema Emmanuel,** KWIMBA

IJUMAA iliyopita, Ilikuwa ni simulizi ya wazee kuozesha mwanafunzi shuleni. Pata simulizi ya ubakaji wa vijana kwenye vichaka vya mtaani:

"Ndoto yangu ilikuwa kuwa mwalimu. Siku moja Jumamosi usiku, ndoto hiyo iliyeyuka kama barafu juani, baada ya kubakwa na kupata mimba.

"Kiukweli sina namna, namwachia Mungu, nahisi kilichobaki ni kuwa mama wa nyumbani," anatamka Paulina Kazimili (siyo jina lake halisi), mwenye umri wa miaka 17, mkazi wa Kijiji cha Njiguja.

Ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule ya sekondari wilayani Kwimba, mtoto wa 11 kati ya 12 katika familia. Anaukumbuka mkasa wa siku Jumamosi, Desemba mwaka jana, giza lilikuwa limeshaaza kutanda, akitoka dukani kununua mahitaji ya nyumbani.

Anasimulia, alipofika eneo lenye kichaka alikutana na kijana ambaye kwa maelezo yake, alishawahi kumhitaji mahusiano lakini yeye hakuwa tayari. Kijana huyo alimvuta vichakani kwa nguvu na kumbaka, wakati huo akisubiri kujiunga na kidato cha kwanza, baada ya matokeo kutoka amefahulu.

### AJIHISI JAMBO

Anasema ni mkasa ambao hakumwambia yeyote kwenye familia akihofia kupigwa. Baada ya shule kufunguliwa, alijiunga kidato cha kwanza, lakini baada ya muda alihisi mabadiliko mwilini, ila hakumueleza mtu.

"Mimba yangu ina miezi saba sasa. Mama yangu kanitambua baada ya shule kusitishwa kwa ajili ya virusi vya Corona. Nilipojitambua nina mimba, sikuacha masomo na hata shuleni hawakujua hadi shule ilipofungwa.



Wanafunzi wa shule za wilayani Kwimba, wakiwa katika mjumuiko wa hafla inayowahusu. **PICHA: MTANDAO.**

> **Ilikuwa Aprili mwaka huu, mtoto alitueleza namna alivyopata ujauzito, tukaamua kutoa taarifa kwa Ofisa Mtendaji wa Kata...**

"Kinachoniumiza, aliyenipa ujauzito alikimbia sijawahi kumuona tena na hajulikani alipo, kwa hiyo mzigo wote umekuwa wa mama yangu ndiye anayenilea maisha yamekuwa magumu kwangu," anaeleza, akitaja baba yake yuko mkoani Kigoma katika nyendo za maisha.

### MAMA YAKE

Martha Joseph, mama mzazi wa Paulina, anaiambia Nipashe, aligundua mimba ya bintiye baada ya kumuona ananenepa na maziwa yanaongezeka, lakini kila alipomuuliza, hakutaka kuongea zaidi ya kuinamisha kichwa.

"Nilipokuwa nikimuuliza kama anaingia hedhi aliniongopea, ndipo niliamua kumbembeleza hatimaye akasema hajaona mzunguko wake. Niliogopa, ikanibidi niende kwa kaka yangu ambaye ni mchungaji kumweleza.

"Ilikuwa Aprili mwaka huu, mtoto alitueleza namna alivyopata ujauzito, tukaamua kutoa taarifa kwa Ofisa Mtendaji wa Kata na suala letu lipo hadi sasa mhusika amekimbia wanaendelea kumtafuta, " anasimulia.

Mama huyo anasema ilikuwa imani yake mtoto angesoma kufikia malengo yake, kwani ana historia ya kufanya vizuri darasani.

Anaendelea: "Mimi sikusoma, nilitegemea mwanangu asome, lakini wanakutana na mambo haya. Nilifanya vibarua ili kuhakikisha mwanangu anasoma, mawazo niliyo nayo nazidi kukonda kila siku."

### SERIKALI WILAYANI

Ofisa Tarafa wa Ngudu, Kwimba, Hamza Hussein, anakiri kuwapo matukio ya wasichana kubakwa, hali inayochochewa na anayoyataja malezi duni, uhuru uliopitiliza na migogoro ya wazazi.

Anasema mpaka sasa kuna mabinti watatu waliobakwa wamehifadhiwa nyumbani kwa Ofisa Mtendaji Kata, akiwamo mwenye umri miaka 11, aliyeumizwa na kudhalilishwa vibaya.

"Ukiangalia mazingira yaliyofanya mpaka jambo hilo likamtokea huyo mtoto ni malezi duni aliyopewa na bibi yake. Marafiki waliokuwa wakienda kumsalimia bibi huyo ndiyo mwisho wa siku wakambaka mjukuu wake," anafafanua.

Mkuu wa Wilaya ya Kwimba, Senyi Ngaga, anasema wamedhamiria kuzimaliza mimba kwa wanafunzi, kwa kuhakikisha zinazoripotiwa wilayani humo na kuzifikisha kwenye vyombo vya sheria, ili zikatolewe uamuzi sahihi.

### WADAU WACHANGIA

Mchungaji wa Kanisa la Pentecostal Assemblies of God Tanzania, wilayani Ngudu, Elias Shileka, anaitaka jamii kulikubali neno la Mungu katika kudumisha maadili kwani ni kinga itakayowasaidia kupitia kumheshimu, Mungu.

Ofisa Tathimini na Ufuatiliaji Mradi wa 'Boresha' wa Shirika la Tanzania Interfaith Partnership (TIP), Kwimba, Respectson Akyoo, anasema wako katiia mapambano kuhakikisha mtoto anapata ulinzi na usalama dhidi ya ukatili wa kingono kwao.

Anasema, mradi ulianza Oktoba mwaka jana na wamesharipoti mikasa 100 inayohusu ukatili wa kingono kwa watoto, wakibaini sababu kuu inajumuisha umaskini, taarifa kutotolewa na hofu ya waathirika, pia imani za kishirikina.

AFYA

# Mapishi ya kuni yanavyowaua macho kinamama wa Zanzibar

• Aliyekutwa asimulia madhila yake; vita ya afya kuhamia nishati gesi

**NA Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWANAISHA Khamis (30) anasumbuliwa na ugonjwa wa macho kwa miaka mitano sasa. Analalama chanzo chake ni moshi unaotokana na matumizi ya kuni kwa ajili ya kupikia.

Mwanaisha, mama wa watoto wawili mkazi wa Kitogani wilayani ya Kusini Unguja, licha ya kuhangaika katika hospitali mbalimbali kutafuta tiba, bado tatizo halijaondoka.

Anasema macho yake huvimba na kutokwa machozi kwa wingi kila anapotumia kuni, lakini kwa sababu ya umasikini na kushindwa kumudu gharama za gesi, anaendelea kutumia nishati hiyo.

"Nasumbuliwa na macho kwa zaidi ya miaka mitano sasa. Nilishatembelea hospitali mbalimbali kutafuta matibabu, lakini bado sijapona na kila ninapotumia kuni kupikia, nazidi kupata maumivu makali," anasema.

Kimsingi, yumo katika orodha ya wanawake wa vijijini wanaoendelea kuathiriwa na maradhi hayo, kutokana na matumizi ya kuni na kutomudu gharama za gesi.

Mkazi wa kijiji cha Muyuni Mkoa wa Kusini Unguja, Saida Rashid (29), amefunga ndoa miaka miwili iliyopita, lakini alikuta nyumbani kwake kuna jiko la gesi.

Anasema, maisha ya kutumia gesi kwa ajili ya kuandaa chakula cha familia yake yamekuwa ya kawaida kwake na hayampi tatizo la kiafya akiwa na ufafanuzi:"Matumizi ya gesi ni mazuri, nafurahia, huchafuki. Pia, unaandaa chakula kwa wakati.

"Katika kipindi cha miaka miwili sasa kwenye ndoa, sijawahi kubaini tatizo lolote la kiafya, tofauti kama ningekuwa natumia kuni"

### WATAALAMU AFYA

Wataalamu wa afya na mazingira wamekuwa wakisisitiza matumizi ya nishati mbadala kama gesi na umeme kwa ajili ya kupikia, kwa sababu yanapunguza asilimia 80 ya uwezekano mtumiaji kupata matatizo ya kiafya na uchafuzi wa hewa.

Mkuu wa Kitengo cha Afya Mazingira, kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Forongo Mtande, anakiri matumizi ya kuni kwa ajili ya kupikia, ni moja ya vyanzo vya maradhi hasa saratani ya koo, moyo, niumionia, kifua kikuu na matizo ya moyo.

Forogo anasema, moshi unaotokana na kuni kiafya ni sumu hasa pale uinapopenya mwilini kwa binadamu, ingawa athari zake zinaweza kujitokeza baada ya muda mrefu na kuna wakati alishuhudia athari zinazotokea ndani ya muda mfupi kwa mtumiaji.

"Kuna sababu nyingi zinazochangia maradhi ya macho, lakini mojawapo ni matumizi ya mara kwa mara ya kuni kwa ajili ya kupikia na tatizo hilo lipo zaidi vijijini, ambako matumizi ya nishati hii ni makubwa kuliko vijijini," anasema.



Mtumiaji kuni akiwa mbele ya mzigo wake ulikokusanywa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**



Mapishi ya kuni yakiendelea. **PICHA: MTANDAO**

> **Tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya gesi na umeme kwa ajili ya kupikia, kwa sababu ni salama na madhara yake ni madogo.**

Mtande anasema moshi unapoingia kwenye macho, huwasha na kuwa mekundi, huku ukitoa machozi na kuna wakati mtumiaji anapata tatizo la kutoona vizuri, pale anapochelewa kupatiwa matibabu.

Anasema hilo ndilo linalofanya Wizara ya Afya ndani ya SMZ kuhamasisha matumizi ya gesi au umeme, kwa sababu ni salama na athari zake kiafya kwa mtumiaji ni ndogo ikilinganishwa na kuni.

"Tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya gesi na umeme kwa ajili ya kupikia, kwa sababu ni salama na madhara yake ni madogo," anafafanua.

Hadi sasa kunatajwa changamoto za kumudu gharama ya gesi na katika baadhi ya vijiji, huduma hiyo haipatikani licha ya jamii kuwa na uwezo wa kununua.

Matumizi ya kuni sio tu yana madhara ya kiafya kwa mtumiaji, lakini pia yamethibitishwa kuwa chanzo kikuu cha uchafuzi wa hewa.

### ULINZI AFYA/ MAZINGIRA

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, Sheha Juma Mjaja, anasema moshi unatokana na kuni, unachafua mazingira na kuharibu hewa safi.

"Moshi unatokana na kuni unapokutana na hewa hugeuka kuwa sumu hivyo unaweza kuwa hatari kwa mazingira yetu, wanyama na hata binaadamu," anasema.

Majaja anawashauri wananchi kuachana na matumizi ya kuni na badala yake, watumie nishati mbadala na hasa gesi kwa ajili ya kupikia. Hata hivyo, licha ya jamii kuwa na hamasa kubwa kutumia gesi ili kupunguza athari za kiafya, bado usambazaji wake unakabiliwa na changamoto.

Omar Ali Yussuf, Ofisa Mwandamizi wa Uchumi na Masoko kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), anasema kitendo cha Zanzibar kutegemea soko la gesi kutoka Tanzania Bara, kunaathiri usambaji wa ndani hali inayosababisha maeneo mingi kutofikiwa na huduma hii.

"Hatuna takwimu sahihi za matumizi ya gesi kwa wananchi, lakini hamasa imekuwa kubwa; watu wengi wanaendelea kutumia gesi kutokana na udhibiti wa matumizi ya kuni na mkaa lakini bado kuna changamoto hasa vijijini, matumizi yako chini," anafafanua.

Yussuf anasema, hilo linathibitishwa na kuongezeka uagizaji wa gesi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kutoka tani 300 kwa mwaka hadi zaidi ya tani 4,000 kwa mwaka za sasa.

"Wastani wa kila kaya tano, kaya mbili zinatumia gesi hasa mijini hivyo mwamko unaanza kuongezeka siku hadi siku," anasema.

Hata hivyo, anataja tatizo kubwa linalochangia kushuka matumizi ya gesi vijijini, ni pamoja na uelewa mdogo wa matumizi ya nishati hiyo na upungufu wa vituo vya usambazaji.

"Tunaendelea kuwekeza katika miundombinu ya gesi ikiwemo kujenga bandari kuhakikisha katika miaka mitano ijayo kaya nne kati ya kila tano iwe inatumia gesi, ili kupunguza uharibifu wa mazingira. Tunaamini uwekezaji huu ukikamilika matumizi ya gesi Zanzibar yatakuwa makubwa," anasema.

Yussuf anawashauri wawekezaji katika sekta hii katika kipindi hiki ambacho miundombinu ya kuhifadhia gesi inaendelea kujengwa, watanue biashara yao vijijini kwa sababu kuna watu wengi wanaohitaji gesi.

AFYA

MWAKA 1937 HADI LEO...

# Kituo kinacholea wenye mazingira magumu 'wastaafu' wao waungana

**Na Christina Haule, Morogoro**

• Wazee wasiowajua wazazi, kituo Mgolole ndio kila kitu



Kundi la kinamama wa Katoliki wakiwa kwenye picha ya pamoja na watoto yatima, baada ya kuwakabidhi misaada. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

HADI sasa ina umri unaokaribia karne moja. Ni tangu ilipoazishwa mwaka 1937 na hadi kufika leo Kituo cha Kulea Watoto cha Mgolole, kina zaidi ya watoto 2000 waliopitia hapo wakiendelea na maisha kwingineko.

Sista Evalister Bunga, Mkuu wa Kituo anasema hadi sasa kuna jumla ya watoto 48, kati yao 11 wenye elimu ya msingi, wengine umri chini ya miaka mitano, wakiwamo watoto wachanga wanne.

Sista Bunga anasema, watoto waliopo kituoni ni zao la changamoto zilizowakuta wazazi. Hapo anataja baadhi, wazazi walifariki baada ya kujifungua na wanapopelekwa kwa ndugu, baada kutimiza taratibu za ustawi wa jamii.

Pia, kiongozi huyo anataja mikasa ya wazazi kuwa watumiaji wa dawa za kulevya, ikiwamo bangi na kuna wazazi wenye matatizo ya akili na wamekosa msaada mbadala.

Sista Bunga anashukuru juhudi zinazofanywa na baadhi ya waliopitia kituo hicho na sasa wakubwa kiumri, ambao wanajitoa kuipa thamani kwamba ni nyumbani kwao. Wanapatembelea na kufanya shughuli mbalimbali na wahudumu wa kituo.

**WALIOPITIA WAONGEA**

Mkuu huyo wa kituoa, anajivuna kwa mfano mmojawapo kwamba aliyekuwa mtoto wa kituoni hicho na sasa mstaafu wa Jeshi la Polisi, Sebastian Usinianze, huwa hachoki kufika mahali hapo.

Ni mwepesi kusaidia malezi ya watoto, hata kuwafanya wasijione wapweke, vivyo hivyo ndivyo inavyofanywa na mashirika, pia taasisi za kidini.

Filbether Kunambi (54), aliyelelewa katika kituo hicho, anasimulia kwamba alifikishwa kisa chake kwamba alifikishwa hapo, akiwa na umri wa miezi mitatu, baada ya mama yake kujifungua na kufariki dunia na ndugu zake walikosa kiwa hawana uwezo wa kusaidia mahitaji yake.

Anasema kutokana na uwepo wa watoto wengi wanaookotwa baada ya kutupwa na kinamama, hali inakuwa mbaya kwa wazazi, kwani baadaye huwakataa kabisa wazazi wao au ndugu pindi wanapojitokeza kuwahitaji.

"Ninashughulika hapa kituoni kama fundi wa kushona nguo za watoto, pia mlezi kwa wadogo zangu hapa kituoni. Nimeshuhudia watoto wanapokuwa wakubwa wakikataa wazazi wao na pengine hata kufikia kuolewa hapa kituoni," anasema Kunambi, katika ufafanuzi wake.

**KINAMAMA WAFADHILI**

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Wakatoliki (WAWATA) kutoka Kigango cha Utatu Mtakatifu, Parokia ya Mtakatifu Monica, Involata Mwagama, anasema msaada huo ni sehemu ya mapendo kutimiza anachokitamka kupitia imani 'matendo ya huruma' kutoka kwao.

> "Si vyema kuwaacha wahitaji wakikosa misaada, jambo ambalo ni hatari na linaweza kusababisha magonjwa na hatimaye vifo kwao... tuwe na mioyo ya kusaidia... kwa kumtukuza Mungu.



Sista Mkuu wa Kituo cha Mgolole, Evalister Bunga, akishukuru msaada waliopata kutoka kwa kinamama wa Kikatoliki (WAWATA), Parokia ya Kihonda, Morogoro.

Katibu wa WAWATA Kigango cha Utatu Mtakatifu, Winifrida Haule, anataja vitu walivyopeleka Mgolole ni vyakula: Juisi na pipi katoni tatu kila moja; sukari kilo 10; maziwa ya watoto wachanga kopo nane; samaki wabichi sangara kilo 25; na vitunguu maji kilo 10.

Vingine anavitaja kuwa mchele kilo 12; ngano kilo 50; mafuta ya kula lita 20; karoti kilo 15; pipili hoho kilo 10; nguo na viatu vya kinamama; pampasi dazeni moja, sabuni za maji lita 10 na miche katoni mbili, misada yote ina thamani ya Sh. 750,000.

**WALENGWA WAFUNGUKA**

Kijana Rey Juma (21), anawashauri wanawake na wasichana kuacha tabia za kutoa mimba au kutupa watoto, akilifananisha na tendo analoliita 'kumkataa Mungu.'

Juma anawaasa kinamama inapotokea wananajikuta wameachwa au kutelelekezwa wasiwakimbile mbadala wa kutupa watoto, bali watafute msaada kwingineko ili wafanikishe malezi ya watoto wao.

"Licha ya kuwa wengi wa vijana wenye tabia mbaya ndio chanzo cha wasichana kutupa watoto, mimi sitafanya hivyo, kwa sababu yule mwanamke anapomtupa mtoto ni sawa na kusema 'unamkataa Mungu' kwa maana ya kukataa kile anachokupa," anasema Juma.

**NENO LA PAROKO**

Padre Octavian Msimbe, wa Parokia ya Kihonda, anawashauri waanzilishi wa vituo vya kusaidia, wahitaji wakiwemo yatima, wazee, wajane na wagane kuvitangaza baada ya kuvisajili, ili iwe rahisi kutambulika na kupatiwa misaada.

Baba Msimbe anasema, hivi karibuni alipata tetesi ya kuwapo kituo cha kulea wazee jirani na Mgolole wanahitaji msaada, jambo analolipa shaka huenda vipo vingine visivyojulikana na wakati huo huo, vinahitaji misaada.

"Si vyema kuwaacha wahitaji wakikosa misaada, jambo ambalo ni hatari na linaweza kusababisha magonjwa na hatimaye vifo kwao... tuwe na mioyo ya kusaidia... kwa kumtukuza Mungu," anasema Paroko Msimbe.

Anasema ni vyema vituo hivyo vikajenga kanuni ya kupita kujitangaza kwenye taasisi za kidini na wadau wengine wa maendeleo, ili kuona uwezekano wa kuwasaidia.

AFYA

# Dk. Leyna: Madini joto shida kubwa katika lishe ya umma

• Jitihada kitaifa zagota 60%; ukichezea tu ujauzito, ukuaji 'umeumia'



Sehemu ya machimbo ya chumvi, Uvinza mkoani Kigoma. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mary Geofrey**

UPUNGUFU wa madini joto imo katika katika matatizo makuu ya lishe nchini. Inashika nafasi ya tatu kwa ukubwa katika matatizo ya lishe, ikitanguliwa na upungufu wa nishati na utomwili (protoni) na upungufu wa wekundu wa damu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Chakula Tanzania (TFNC), Dk. Germana Leyna, anasema tatizo hilo linaathiri afya na maendeleo ya jamii, ikiwa ni pamoja na uzalishaji mali na uchumi.

Anasema madhara yatokanayo na upungufu wa madini joto ni mengi na yanaathiri makundi mbalimbali katika hatua za ukuaji kuanzia ujauzito, utoto, ujana na utu uzima.

"Athari hizi ni pamoja na kuharibika mimba, kuzaa mtoto mlemavu, uvimbe wa tezi ka shingo, udumavu, ulemavu na akili na mwili," anaeleza Dk. Leyna.

Anasema mikakati ya kuzuia upungufu wa madini joto nchini, ilianza kwa kuhusisha matibabu kwa kutumia vidonge, matone na sindano za madini joto kama mkakati wa muda mfupi. Dk. Leyna anasema kutokana na mkakati huo kuwa wa gharama kubwa na usio endelevu, mwaka 1994, mkakati wa kuweka madini joto kwenye chumvi ulianzishwa katika namna endelevu na ya kudumu.

Anasema, mkakati huo wa uwekaji madini joto kwenye chumvi huliwa na watu wengi kila siku kwa kiasi kisichotofautiana, teknolojia na vifaa vinavyotumika katika kuchanganya chumvi na madini hayo, ni rahisi chumvi iliyowekewa madini haibadiliki rangi, harufu wala ladha yake. Anaeleza kuwa bei ya chumvi hiyo ni nafuu, ikilinganishwa na vyakula vya chumvi, vinatumiwa kama njia ya kufikishia madini joto hayo kwa mlaji.

> **Sheria hii Kuu ya Madini ya Mwaka 1979 na ile ya Chakula ya Mwaka 1978, vifungu hivi vimefanyiwa mapitio mwaka 2003 na kuwa kanuni mwaka 2010.**



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Chakula na Lishe, Dk. Germana Leyna. **PICHA: BLOGU YA SERIKALI**

**CHUMVI INAVYOTUMIKA**

Dk. Leyna anasema, takwimu kitaifa za matumizi ya chumvi yenye madini joto, yanaonyesha kaya zinazotumia chumvi hizo zimeongezeka kutoka asilimia 90 hadi 96.4.

Aidha, kaya zinazotumia chumvi yenye madini joto toshelevu zimeongezeka kutoka asilimia 47 hadi asilimia 61, ila changamoto kubwa katika mikoa inayozalisha chumvi kwa sababu kaya zinazotumia chumvi bado zipo kwa ngazi ya chini. Daktari huyo anasema, taasisi hiyo imekuwa ikifanya mikakati ya kuhakikisha chumvi yenye madini joto toshelevu, inapatikana kwa wingi.

Anataja mikakati hiyo, ni kutoa mafunzo kwa maofisa afya na wazalishaji wa chumvi kuhusu umuhimu wa madini joto mwilini na madhara yatokanayo na upungufu wa madini, uzalishaji chumvi bora na yenye madini joto na ufuatiliaji wake.

Vilevile, anasema wanahamasisha viongozi wa kamati za ulinzi na usalama katika ngazi zote kutoa elimu ya umma kupitia vyombo vya habari na mawasiliano vilivyopo.

**WAANZISHA CHAMA**

Dk. Leyna anasema, wameanzisha Chama cha Wazalishaji wa Chumvi, lengo kuu likiwa ni kuwaunganisha wazalishaji chumvi na wadau wengine, ili kuwapo yzalisha chumvi bora yenye madini joto yanayojitosheleza.

Ahadi nyingine, ni kwamba wanadhamiria kuhakikisha uzalishaji wa chumvi yenye madini joto na upatikanaji madini joto kwa namna mbalimbali.

Mkakati mwingine anaoutaka ni kuwapo kwa Kamati ya Kitaifa inayoratibu mpango wa kudhibiti upungufu wa madini joto yenye uwakilishi kutoka sekta mbalimbali. Dk. Leyna anasema, walianzisha Sheria ya Chumvi iliyopitishwa bungeni mwaka 1994, ili kusimamia na kuhakikisha kuwa chumvi yote inayozalishwa au kuingizwa nchini kwa matumizi ya binadamu na wanyama, imechanganywa na madini joto.

"Sheria hii Kuu ya Madini ya Mwaka 1979 na ile ya Chakula ya Mwaka 1978, vifungu hivi vimefanyiwa mapitio mwaka 2003 na kuwa kanuni mwaka 2010," anaeleza Dk. Leyna.

Anasema taasisi ya Chakula na Lishe, kwa kushirikiana na wadau wa chumvi, ilisambaza mashine za kupima kiasi cha madini joto kwenye chumvi katika halmashauri zote zinazozalisha bidhaa hiyo nchini.

Mtaalamu huyo anasema wamekuwa wakiwafuatilia kila mara wazalishaji na wauzaji chumvi katika maeneo yote nchini, kupata picha halisi ya mwenendo walio nao.

"Vilevile wauzaji na wasambazaji wakubwa na wadogo walipatiwa mafunzo kuhusu umuhimu wa kuuza chumvi yenye madini joto yenye ubora katika baadhi ya halmashauri nchini," anaeleza Mkurugenzi huyo.

Dk. Leyna anasema, mwaka 2016 taasisi hiyo kwa kushirikiana na wadau, walifanya mapitio ya mkakati wa uongezaji wa madini joto kwenye chumvi na kubainisha changamoto zilizopo katika sekta hiyo.

Anasema tathimini ilibaini uwapo wa wazalishaji wa chumvi wengi wadogo wadogo na kati katika maeneo ambayo hawayafikii kirahisi na wanaozalisha chumvi isiyo na ubora. Pia, kuna suala la kushindwa kuanzisha biashara zenye faida kiuchumi na matumizi ya teknolojia duni katika kuweka madini joto kwenye chumvi.

Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na tathimini hiyo, Dk. Leyna anayataja ni kuandaa miundombinu inayojumuisha wazalishaji chumvi wadogo, wa kati na wakubwa, kufanya utafiti katika sekta ya chumvi ili kupata maelezo ya kina kuhusu uandaaji miundombinu ya wazalisha chumvi nchini, ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji bora wenye madini joto.

Dk. Leyna anasema, katika kuwasaidia wazalishaji chumvi waweze kuzalisha kwa ubora yenye madini joto, mwaka 2019 taasisi kwa kushirikiana na wadau ilisambaza mashine za usalishaji wa madini joto katika baadhi ya halmashauri nchini.

Anataja baadhi ni Kilwa, Meatu na Hanang, akianisha sababu zake ni pamoja na maeneo hayo kuzalisha chumvi nyingi, lakini isiyo na madini joto.

Pia, anataja kuwa wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa matumia ya chumvi yenye madini joto, ili kuepuka madhara yatokanayo na tatizo hilo.

Anasema, pia wanaelimisha jamii kuhusu uhifadhi sahihi wa chumvi yenye madini joto kwenye kaya na kuelimisha wazalishaji, wasambazaji na wauzaji kuhusu uuzaji na uhifadhi sahihi wa chumvi yenye madini joto.



# TAKUKURU yashtukia rushwa mkutano wa chama cha wafugaji

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, imeanza kufanya uchunguzi wa viashiria vya rushwa katika uchaguzi mkuu wa Chama cha Wafugaji nchini unaotarajiwa kufanyika Julai 19, mwaka huu.

Akizungumza na jana na waandishi wa habari, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema wamepata taarifa za uwapo wa viashiria hivyo na wameanza uchunguzi ili kuwachukulia hatua watu watakaobainika kutoa au kupokea rushwa.

Kibwengo alisema wamebaini kwamba wapo baadhi ya wagombea ambao wanatumia ushawishi wa fedha kwa kuwalipia ada za uanachama wafugaji ili wapate sifa za kupiga kura, hivyo kutumia rushwa ili wao au wagombea wanaowaunga mkono wapigiwe kura.

"Tumeanza uchunguzi na kupitia uchunguzi huu tumebaini kuna magenge ya watu ambao wamedhamiria kutumia ushawishi wa rushwa ili kuvuruga uchaguzi," alisema.

Aliongeza: "Vitendo hivyo vyote ni vya kijinai na havitavumilika hata kidogo katika mkoa wetu wa Dodoma na Tanzania kwa ujumla." Aidha, alisema aliwataka wagombea na wapambe wao kutambua kuwa TAKUKURU Dodoma ipo imara na imejipanga vyema kukabiliana na vitendo vyovyote ambavyo ni kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007. "Tunafuatilia nyendo za watu hao na tutachukua hatua stahiki baada ya kujiridhisha kwa uwepo wa ushahidi kwa wote wanaojihusisha na vitendo hivyo," alisema.

Aliwasihi wafugaji na wananchi kwa ujumla kutoa taarifa ya vitendo vya rushwa ili wapate viongozi wasiotokana na rushwa. "Taarifa yoyote kuhusu vitendo vya rushwa wakati wa kampeni na kuelekea siku ya uchaguzi wa viongozi wa chama cha wafugaji ngazi ya kitaifa ziwasilishwe kupitia simu ya bure 113 au kwa kufika kwenye ofisi za TAKUKURU," alisema.

Alisema lengo lao ni kuona uchaguzi huo unakuwa wa uhuru na haki ili kila mmoja ashinde kulingana na uwezo wa kiutendaji aliokuwa nao.

Aliwasisitiza wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU ili kusaidia kukomesha vitendo vya rushwa katika sekta mbalimbali.



Wakazi wa eneo la Mbuyuni, Kata ya Kizota, jijini Dodoma, wakiwa wamekusanyika walipokutana na waandishi wa habari, hivi karibuni, kutoa malalamiko yao kuhusu eneo ambalo wanadai walinyang'anywa na uongozi wa jiji hilo, bila ya kulipwa fidia.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# UWT yawatoa hofu wagombea viti maalum

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

JUMUIYA ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi Tanzania (UWT), imewatoa hofu wanawake wote nchini kuwa vikao vyote vya uchujaji wagombea vitazingatia kanuni, taratibu na mwongozo na hakutakuwa na upendeleo wowote.

Sambamba na hilo, imesema katika uchaguzi wa mwaka huu kumekuwa na mwitikio mkubwa wa wanawake waliojitokeza kuchukua fomu kuwania nafasi mbalimbali kupitia chama hicho kutokana na kazi nzuri iliyofanyika na Rais John Magufuli.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake jijini hapa, Katibu wa UWT, Queen Mlozi, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanawatendea haki wanawake wote waliojitokeza.

"Katika mchakato unaoendelea, tumeona mwitikio ni mkubwa sana, mfano Mkoa wa Dodoma siku ya kwanza ya uchukuaji fomu wanawake 50 wamejitokeza kuchukua fomu, nawahakikishia kuwa tutasimamia kanuni za uteuzi za wagombea wa uongozi katika vyombo vya dola," alisema.

Alisema katika kanuni hiyo ibara ya 18 imetoa mwongozo wa mgawanyo wa viti maalum kwa makundi ya wabunge wanawake kutoka katika mikoa, kundi la wafanyakazi, wasomi, mashirika yasiyo ya kiserikali (NG'Os) na watu wenye ulemavu.

Aliongeza kuwa UWT itaendelea kuwapigania wanawake kwa nguvu zote ili kuhakikisha wanakuwa huru.

Mlozi alitoa rai kwa wanawake kuendelea kujitokeza kwa wingi kugombea ili lengo la 50 kwa 50 liweze kufikiwa.

Aliwasisitiza kutoruhusu vitendo vya rushwa na yeyote atakayebainika anahusika na vitendo hivyo sheria itafuata mkondo wake.

Katika hatua nyingine, wagombea wanawake wa udiwani na ubunge walisema wamehamasisha kugombea kutokana na hivyo kuwajengea ujasiri.

Wagombea wa Jimbo la Mtera Happiness Mugongo na Mwanga Chibago, walisema miaka yote wamekuwa hawajiamini na kushindwa kugombea nafasi muhimu za uwakilishi.

# UDP yataka haki uchaguzi mkuu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha UDP kimeitaka serikali kuhakikisha inaweka mazingira ya haki na amani katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Aidha, kimetangaza kuwa kitamuunga mkono, Rais John Magufuli katika uchaguzi huo kutokana na utendaji wake mzuri.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Chama hicho, John Cheyo katika mkutano mkuu wa chama hicho.

"Tunaomba mazingira ya haki na amani, amani ndio msingi wa kila kitu, siasa sio uadui hakuna chama kinaandikishwa kwamba ni chama cha upinzani, tupambane ili tujaze watu wengi bungeni," alisema.

Kadhalika, alisema kikao chao kwa pamoja wamekubaliana kumuunga mkono Rais Magufuli kutokana na utendaji kazi wake kuwagusa kwenye nyanja mambo mbalimbali.

"UDP inamuunga mkono ametupatia heshima kubwa sana, Magufuli anasema sisi sio maskini ni matajiri na UDP tunasema hivyo hivyo sisi ni matajiri... sasa kwa nini tusimuunge mkono, ametuheshimisha sana. Sijasema tumeungana na CCM na sisi tunataka ubunge na udiwani," alisema Cheyo.

Cheyo alivitaka vyama vingine kuiga mfano wao kwa kumuunga mkono Rais Magufuli katika nafasi ya urais kwani mchezo umeishaisha na fedha wanazotoa kwa ajili ya kugombea katika nafasi hiyo ni kama wanazichezea.

"Natoa wito kwa vyama vingine huyu Rais hajakosea, tumuunge mkono kama mtu anatosha sasa 'the game its over' sisi tugawane katika udiwani na ubunge kwani huku ni kupoteza fedha bure Rais Magufuli anatosha kwa kiwango kikubwa sana," alisema.

Alisema wao watagombea katika nafasi za ubunge na udiwani pekee, huku katika nafasi ya urais wakimwachia Magufuli.

"Mwaka 2004 nilikuwa nikiwaambia zaeni tu na elimu itakuwa bure kuanzia darasa la kwanza hadi la kumi na mbili nikachekwa...Magufuli amesikia hilo na mabilioni yanatoka kwa ajili ya elimu kwanini sasa tusimuunge mkono mtu kama huyo?"Alihoji.

Aidha, alisema msimamo wa UDP ni kwamba ardhi ni mali ya mtu mmoja mmoja na kwamba suala la utolewaji wa hati kwa muda wa miaka 33 ni mfumo wa kikoloni ambao unatakiwa kuangaliwa kwa umakini.

"Kuna hati ya miaka 33 hii tulikuwa tunapewa sisi na wakoloni miaka hiyo, Wahindi ilikuwa ni miaka 66 na Wazungu ni miaka 99 tumerithi hili tunatakiwa tulibadilishe, yaani kama unanyumba ulijenga miaka 33 iliyopita sio yako fanya mchakato upewe hati nyingine," alisema.

Alisema wale wanaopewa hati za kimila ndio wapo sahihi inadumu maisha yote ya mtu hivyo serikali inatakiwa kutumia mfumo kama huo katika hati za viwanja vingine.

"Tunataka wapaze sauti wabunge katika hili naamini Rais Magufuli kwa sababu amefanya mengi sana na hili atakuja kuliangalia kwanini hati ikae kwa miaka 33 pekee," alisema.





## Walilia kujengewa barabara

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Ikukwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kukamilisha ujenzi wa barabara ya kupita Mlima Mbeya, ili kupunguza umbali wa zaidi ya kilomita 30 kuzifikia ofisi za makao makuu ya wilaya.

Walipaza sauti zao juzi walipozungumza na Nipashe kuhusu matatizo yanayowakabili kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara inayounganisha kata hiyo na maeneo mengine ya wilaya.

Ashura Mwavilenga, mkazi wa kata hiyo, alisema barabara wanayotumia kwa sasa ni ya kutoka Mkwajuni kwenda Mbalizi ambayo ina umbali wa kilomita 70, lakini wakijengewa ya kupitia Mlima Mbeya, itakuwa na kilomita 40 pekee kufika makao makuu ya wilaya.

Alisema serikali ilishaanza ujenzi wa barabara hiyo, lakini inajengwa kwa kasi ndogo kulinganishwa na mahitaji ya wananchi wa kata hiyo ambayo inategemea huduma nyingi za kijamii katika Jiji la Mbeya na Mji Mdogo wa Mbalizi.

"Tumejengewa kituo cha afya kikubwa ambacho kitaturahisishia huduma za afya, lakini bado tuna tatizo la miundombinu ya barabara kwa ajili ya kuwasafirisha wagonjwa ikitokea dharura," alisema Ashura.

James Amon, mkazi mwingine wa kata hiyo, alisema ujenzi wa barabara hiyo ukikamilika, utawasaidia wananchi kuepukana na tatizo la kutembea umbali mrefu kuitafuta barabara ya Mbalizi-Mkwajuni.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alifanya ziara ya kukagua Kituo cha Afya Ikukwa na aliwapa matumaini wananchi hao kuwa barabara hiyo pamoja na inayounganisha na ile ya Mkwajuni-Mbalizi, zitaboreshwa.

Chalamila alisema hadi sasa, ujenzi wa barabara hiyo umebakia kilomita chache kukamilika, hivyo wananchi wanatakiwa kuendelea kuvumilia kwa kuwa serikali imesikia kilio chao na kuamua kukitatua.

# Kada CCM anaswa klabu ya pombe tuhuma za rushwa

Na Nebart Msokwa, MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, inamchunguza kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini kwa kosa la kuwashawishi baadhi ya wajumbe wa chama hicho wamchague kwenye kura za maoni.

Taarifa ya Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, ilimtaja kada huyo kuwa ni Cosmas Mwaifwani, ambaye ni miongoni mwa waliotia nia ya ubunge wa Mbeya Mjini.

Matechi alisema mwanasiasa huyo alikamatwa na maofisa wa TAKUKURU Julai 12 saa nane mchana akiwa na baadhi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini kwenye moja ya vilabu vya pombe za kienyeji vilivyoko Kata ya Itende.

Alisema kigogo huyo alikuwa anawashawishi wajumbe hao wamchague kwenye kura za maoni za kumpata mgombea atakayepeperusha bendera ya CCM kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

"Tunaendelea na uchunguzi wa tukio hilo na tukishakamilisha taarifa itatolewa, lakini kitendo hicho ni kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007," alisema Matechi.

Aliwashukuru wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa kuendelea kushirikiana na taasisi hiyo kwenye vita dhidi ya rushwa na akawaomba kuendelea kutoa taarifa wanapoona viashiria vya rushwa, ili kuhakikisha vitendo hivyo vinadhibitiwa mapema.

Aliwataka kutoa taarifa za siri kwa kupiga namba za bure za TAKUKURU ambazo ni 113 ama kuandika ujumbe mfupi wa maandishi kwenda namba *113# na kufuata maelekezo.

Aliwataka wananchi kuwaepuka watu wanaoutaka uongozi kwa kutumia rushwa, akifafanua kuwa watakuwa wanajikosesha wenyewe haki ya kuchagua viongozi wao kwa uhuru. Katika kinyang'anyiro cha ubunge ndani ya jimbo hilo, vyama vikuu vinavyochuana vya CCM na CHADEMA, vinaendelea na michakato ya kuwapata wawakilishi katika ngazi hiyo.

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CHADEMA Jimbo la Mbeya Mjini, walipiga kura za maoni juzi ambapo walimpitisha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Joseph Mbilinyi 'Sugu' kwa kura 313 za ndiyo kati ya 318 zilizopigwa.

Kwa upande wa CCM, pazia la wanachama kuchukua na kujaza fomu za kuwania nafasi za ubunge na udiwani lilifunguliwa juzi ambapo wanachama 20 walijitosa siku hiyo kuchukua fomu za kumkabili Sugu kwenye nafasi ya ubunge.

Mmoja wa waliojitokeza ndani ya chama hicho ni Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ambaye alikuwa miongoni mwa watia nia waliokuwa wa kwanza kuchukua fomu hizo.

Tangu mwanzo wa mchakato, TAKUKURU ilitoa tahadhari kwa vyama vya siasa kuepuka kushiriki vitendo vya rushwa na uongozi wa CCM kupitia kwa Katibu wake wa Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, ulishatahadharisha pia wanachama wake kujihusisha na vitendo hivyo.



Mmoja wa maofisa wa kampuni zinazonunua tumbaku katika Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, akikagua mitumba ya zao hilo kwenye moja ya maghala yaliyopo katika Kata ya Lupatingatinga juzi, ambamo yanahifadhiwa kabla ya kusafirishwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC ahamisha vita ya corona kwa malaria

Na Grace Mwakalinga, SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemas Mwangela, ameapa kupambana na ugonjwa wa malaria kama ilivyokuwa kwenye mapambano dhidi ya maambukizi ya corona kwa kuhakikisha mkoa huo unafikisha asilimia sifuri ya maambukizi kutoka asilimia moja ya sasa.

Brigedia Jenerali Mwangela alitoa kauli hiyo jana alipofungua kampeni ya kutokomeza malaria mkoani humo, akisema vita ya malaria inahitaji nguvu kubwa na muda.

Alisema kwa sasa mkoa huo una asilimia moja ya maambukizi ya ugonjwa wa malaria na kwamba lengo sasa ni kuimaliza kabisa kwa kuhakikisha wanaangamizi mazalia ya mbu yanayopatikana kwenye maji yaliyotuama ama mitoni.

Aliongeza kuwa mafunzo ya waliopatiwa wananchi juu ya namna ya upuliziaji wa dawa hizo za kutokomeza malaria na elimu ya kuhamasisha vita hiyo yatakuwa chachu ya kuongeza nguvu katika mapambano.

"Ninafurahi kuona mkoa wetu ni mmoja ya mikoa ya kwanza kuzindua kampeni hii, tunawahakikishia kuwa ugonjwa wa malaria utakuwa wa kihistoria hapa kwetu. Jambo la muhimu kwa sasa ni kuwaandaa wakurugenzi kufika kwenye kiwanda cha Shirika la Maendeleo (NDC), kuchukua dawa ya kuua mazalia ya mbu," aliagiza.

Brigedia Jenerali Mwangela pia aliiomba NDC pamoja na Shirika la Kumekucha ambao wanaendesha kampeni ya kutomeza malaria, kupanga bei rafiki ili kila mwananchi amudu gharama za dawa hizo.

Mkurugenzi wa Shirika la Kumekucha, Jackson Cyprian, alisema waliamua kuanzisha kampeni hiyo, ili kumaliza kabisa ugonjwa wa malaria nchini kwa sababu kiwanda cha kuua viuadudu vinavyosababisha ugonjwa huo kipo nchini eneo la Pwani.

Alisema kiwanda hicho ni cha pekee barani Afrika na kinaweza kuzalisha dawa nyingi, ili kuua viuadudu vinavyozalisha mbu wanaoeneza malaria.

"Ugonjwa wa malaria utakwisha na itabaki historia tu. Ninawaomba Watanzania tuunge mkono jitihada za Rais John Magufuli ambapo tangu mwaka 2017 aliagiza kuanza mchakato wa kumaliza ugonjwa huo ambao umeua maelfu ya Watanzania," alisema Cyprian.

Aliongeza kuwa lengo ni kuhakikisha hadi kufikia mwaka 2025, ugonjwa wa malaria unaisha kabisa na ibaki historia na kuwashauri Watanzania kutokubali kurubuniwa na wachache ambao hutumia ugonjwa huo kujipatia pesa.

Kampeni ya kutokomeza malaria nchini ilianza mkoani Mbeya ikipita pia katika mikoa ya Songwe, Ruvuma na Morogoro yenye idadi ndogo ya maambukizi ya ugonjwa huo ili kumaliza kabisa maambukizi na kisha kufikia mikoa mingine.

Makamu Meneja wa Uzalishaji wa Kiwanda cha Viuadudu cha NDC kilichoko Kibaha mkoani Pwani, Gasper Philip, alisema tangu kianzishwe, nchi mbalimbali zinatumia dawa zake.

Ofisa Mwandamizi wa Shirika hilo, Dorice Rutina, alisema dawa hizo zinauzwa kwa bei nafuu ambayo ni rafiki kwa kila Mtanzania ya kuanzia Sh. 1,000 hadi 15,000.





Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad (kushoto), akirejesha fomu ya kugombea urais wa Zanzibar kupitia chama hicho, (kulia) ni Naibu Mkurugenzi wa Kampeni na Uchaguzi wa chama hicho, Muhene Said Rashid. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Maalim Seif arejesha fomu urais Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amerejesha fomu ya kuomba ridhaa ya kuwania urais wa Zanzibar kupitia chama hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kurejesha fomu hiyo jana, Maalim Seif alidai bado kuna tatizo la wananchi wengi kutopata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, hivyo kuwa hatarini kukosa kutojiandikisha katika daftari la wapigakura.

Maalim Seif alisema licha ya kuwapo kwa dosari hiyo, anaamini watashinda katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Alisema wananchi wana imani na chama hicho, hivyo hawana wasiwasi katika suala la ushindi.

Maalim Seif alikabidhi fomu hizo kwa Naibu Katibu Mkuu wa Kampeni na Uchaguzi, Muhene Said Rashid, katika ofisi za ACT-Wazalendo zilizoko Vuga mjini Zanzibar. Naibu Katibu Mkuu huyo alisema kuwa, hadi jana hakuna mwanachama mwingine alijitokeza kugombea nafasi hiyo ya urais wa Zanzibar.

"Zoezi la uchukuaji na urejeshaji fomu mwisho ni Julai 20 mwaka huu, na hadi sasa ni Maalim Seif Sharif pekee ndiye aliyechukua fomu ya kugombea urais wa Zanzibar," alisema Rashid.

# Wanachama 120 CHADEMA Zanzibar wajitosa kusaka ubunge, uwakilishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA Kanda ya Unguja, kimesema wanachama wengi wamejitokeza kuchukua fomu ya kuomba ridhaa kwa chama kuchaguliwa kuwa wagombea wa nafasi za uwakilishi na ubunge katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Unguja, Said Mzee Said, alisema mchakato wa uchukuaji wa fomu kwa nafasi ya uwakilishi na ubunge ulianza Julai 4 na unatarajiwa kumalizika Julai 10 mwaka huu.

Alisema katika mchakato huo, wanachama 58 wamejitokeza kuchukua fomu ya ubunge na 61 wamejitokeza kuchukua fomu ya uwakilishi kwa majimbo yote ya Unguja na Pemba.

"Kwa Unguja pekee, majimbo yote ya uchaguzi ambayo ni 32, wanachama wamejitokeza kuchukua fomu za kuomba ridhaa kuchaguliwa na chama chetu kugombea nafasi ya uwakilishi na ubunge," alisema.

Said alisema kwamba, mwaka huu mwitiko ni mkubwa kwa wanachama hao kujitokeza kuchukua fomu kulinganisha na miaka iliyopita. "Kundi kubwa la vijana, wanawake kwa mwaka huu wamehamasika kuchukua fomu za kuomba ridhaa katika chama chetu kuteuliwa kuwa wagombea ambao watatuwakilisha katika Uchaguzi Mkuu," alisema Said.

Aliongeza kwamba, baada ya kukamilika kwa uchukuaji fomu, vikao mbalimbali vya kamati maalum za chama hicho vilianza jana kwa lengo la kuwajadili na kuwachuja wagombea hao.

Said alibainisha kuwa uchukuaji wa fomu za udiwani kwa wadi zote Unguja na Pemba unaendelea baada ya kuanza Julai 11 na unatarajiwa kufikia tamati Julai 17 mwaka huu.

Alisema baada ya kukamilika kwa uchukuaji fomu hizo, kura za maoni na kamati tendaji kanda kuanzia Julai 20 hadi 23 na Julai 24 kamati tendaji kuteuwa wagombea wa nafasi hiyo.

## ZEC kutoa vitambulisho wapigakura

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), inatarajia kuanza kutoa vitambulisho vipya vya kupigia kura kwa wananchi Julai 18, mwaka huu.

Tume hiyo itatoa vitambulisho hivyo kwa vituo vyote 407 vilivyotumika kwa kazi ya uandikishaji wapigakura wapya na uhakiki wa taarifa za wapigakura Unguja na Pemba. Akitoa taarifa kuhusiana na kazi hiyo jana, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa ZEC, Thabit Idarous Faina, alisema kazi hiyo inatarajia kuanza Julai 18 na 19 kwa Pemba na kwamba kwa Unguja wataanza Julai 25 mwaka huu.

Mkurugenzi huyo alisema ZEC katika kufikia malengo yake, imepata mafanikio makubwa katika hatua zote za maandalizi ya uchaguzi ikiwamo uandikishaji, uwekaji wazi orodha ya wapigakura waliokosa sifa za kuwa wapigakura na orodha ya wapigakura wapya.

"Mpaka sasa, hakuna malalamiko au pingamizi ya mtu yeyote iliyojitokeza katika orodha ya wapigakura wapya," alisema Faina.

Akizungumzia kuhusu mwongozo wa uchukuaji wa vitambulisho vya kupigia kura, alisema kazi hiyo itafanyika kwa mujibu wa sheria na utaratibu uliwekwa na tume kwa kuwapatia wananchi vitambulisho vyao waliomo katika daftari la wapigakura.

Aliwataka wananchi kufika vituoni kuchukua vitambulisho hivyo ili kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu.

Aliwataka wananchi hao watakaoenda kuchukua vitambulisho hivyo vipya kuhakikisha kuwa wanachukua na risiti walizopewa awali wakati walipoenda kujiandikisha pamoja na kitambulisho na Mzanzibari Mkazi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

ROCK TAKERS LTD

158135

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**SHAURI LA MADAI NO 85/2019.**
**PUNUNTAS COMPANY LTD**
**(NEWTON KITUNDU)................MDAI**
**DHIDI YA**
**CECILIA LUCAS..........MDAIWA**

KWA IDINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA WILAYA YA NYAMAGANA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI YA MDAIWA AMBAYO NI NYUMBA SIKU YA ALHAMISI TAREHE 23/07/2020 KWANZIA SAA SITA MCHANA NA KUENDELEA MNADA UTAFANYIKA MA MAHALI MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA | NCHENGA- NYEGEZI | SAA 6 MCHANA NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. MTEJA ATALIPWA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYO FIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYO SALIA ATAILIPIA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE, KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZO JITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO.0627 672221 AU 0659 570570**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO
TANGAZO LA KUITWA SHAURINI
**SHAURI LA MADAI NAMBA:179..2020**

Mdai: HAME MUSSA
DHIDI YA
Mdaiwa: RASHID ALLYN
Kwa: RASHID ALLY

Ombi la Mdai: HAME MUSSA
Madai ya: PESA Sh. 306,000

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 20 mwezi 07 mwaka 2020 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 09 mwezi 07 mwaka 2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

158131

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;182/2020**

**Ombi la KHALID HUSSEIN SHABAN MISOTI, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ZAINABU ABDALLAH LUBANGO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/07/2020.

Tarehe 14/7/2020
Sahihi ya Hakimu
MOROGORO

115812402

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**LUCY GABRIEL KALINGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 724 DEG IST TOYOTA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya Polisi:
**DAR/OST/RB/526318/2020.**

115812502

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI**

**INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB:**

**+255 - 0782253676**

***Kwa Habari Motomoto***

***usikose Gazeti lako la***

***Nipashe kila siku***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati ya mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARI PICHA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikabidhiwa fomu za kuwania tena ubunge wa Jimbo la Ruangwa na Katibu wa CCM wa Wilaya ya Ruangwa, Barnabas Essau kwenye ofisi ya CCM ya wilaya hiyo, jana. Kushoto ni mkewe Mary Majaliwa. **PICHA: OWM**



Katibu wa CCM Wilaya ya Ilala, Iddi Mkowa, akimkabidhi mwanahabari Angel Akilimali fomu ya kuomba ridhaa ya kuwania ubunge wa Jimbo la Ukonga, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Katibu wa CCM Wilaya ya Tanga, Salimu Kidimba (kushoto), akikabidhi fomu ya kugombea ubunge Jimbo la Tanga Mjini, kwa katibu wa chama hicho, Wilaya ya Kiteto, Shekuwe Pashua katika ofisi ya CCM wilaya jana. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**



Mwanasheria maarufu Albart Msando (kulia), akijadiliana jambo na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Arusha Mjini, Denis Mwita kabla ya kuchukua fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge wa Jimbo la Arusha Mjini, jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Katibu wa CCM Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, Sylvester Yared, akimkabidhi jana fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge katika Jimbo la Kibamba Wakili Erick Kidyalla. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilayani Mbulu, mkoani Manyara, Dinah Samanyi (kulia), akimkabidhi Mkurugenzi wa Tiba wa Hospitali ya Rufani ya Haydom, Dk. Emmanuel Nuwass, fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**




# ZIDANE: HAZARD BADO HAJAWA FITI

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane ameelezea hali ya Eden Hazard pale Real Madrid kama ni ngumu baada ya kumuacha nyota huyo wa Ubelgiji benchi bila kumtumia, wakati wakiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Granada Jumatatu.

Mabao ya mapema ya Ferland Mendy na Karim Benzema yaliipa ushindi Madrid na kujivuta kwenye nafasi nzuri zaidi ya kutwaa ubingwa wa LaLiga.

Hazard aliwasili Chelsea kwa ada ya euro milioni 100 kabla ya kuanza kwa msimu huu, lakini amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara - akiwa amevunjika kifundo cha mguu na kumfanya kupata nafasi ndogo ya kucheza msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, amecheza mechi 15 tu za Ligi Kuu na amecheza dakika nane tu tangu aliporudi dhidi ya Real Mallorca na Espanyol mwishoni mwa mwezi uliopita.

Baada ya ushindi wa tisa mfululizo, Zidane aliwaambia waandishi wa habari kuwa bado Hazard hayupo fiti.

"Kama mchezaji amekuwa kwenye hali nzuri, lakini bado hajapona sawasawa," alisema. "Hali yake kwa kiasi fulani ni ngumu, lakini nina matumani kesho (leo), anaweza kuwa fiti kwa asilimia 100 na kutukusaidia kutwaa ubingwa. Na hicho ndicho anachotaka."

Madrid watawakaribisha Villarreal leo, wakijua kwamba ushindi utawawezesha kutwaa taji la Ligi Kuu ya Hispania msimu huu.

# Guardiola: Mkataba mpya subirini kwanza

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anaamini sasa si muda wa kujadili kuhusu mkataba mpya pale Manchester City – ingawa amesisitiza angeweza kubaki klabuni hapo hata kama ingeshushwa hadi Ligi Daraja la Pili.

Jumatatu mahakama ya usuluhishi wa michezo iliifuta adhabu ya Man City kufungiwa miaka miwili kutocheza mashindano ya Ulaya na faini ya euro milioni 30, baada ya kuvunja sheria ya haki ya usawa kwenye usajili wa wachezaji, iliyotolewa na Shirikisho la Soka Ulaya, Uefa.

City bado wapo kwenye nusu fainali ya Kombe la FA ambapo itacheza na Arsenal na pia mchezo mmoja wa hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid, huku msimu wa 2020-21 utamfanya Guardiola kwa mara ya kwanza kuwa na klabu moja kwa misimu mitano.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana Jumatano dhidi ya Bournemouth kwenye Ligi Kuu, alisema sasa si muda wa kuzungumzia mkataba mpya.

"Hakuna kilichobadili mtazamo wangu, pengine nitakuwa na uwezo wa kukaa hapa kwa muda mrefu zaidi," alisema Guardiola wakati alipoulizwa kama atasaini mkataba mpya.

"Kama ni klabu na taasisi, watu hawaelewi namna gani ulikuwa wakati mgumu kwa watu wote klabuni, kuwa kwenye hukumu ya kitu ambacho hatukukifanya.

"Matumaini yangu watu wanaweza kuacha kuzungumza kuhusu hili au wanaweza kwenda mahakamani kuthibitisha kama tulifanya hivyo."






# Matic: Pogba atabakia Utd

**MANCHESTER,** England

NEMANJA Matic ana imani kubwa Paul Pogba atabaki na Manchester United "kwa muda mrefu."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia amekuwa na upatina mzuri kwenye nafasi ya kiungo pamoja na Pogba na Bruno Fernandes tangu kuzaliwa upya kwa miamba hao kwenye Ligi Kuu, na kuwasaidia United kutopoteza katika mechi 18 kwenye mashindano yote.

Majaliwa ya Pogba pale United kwa muda mrefu yanaonekana kuwa shakani, huku wakala wake, Mino Raiola akidai kwamba mteja wake ataondoka mwishoni mwa msimu huu.

Lakini Matic anafikiri mchezaji mwenzake huyo sasa anafurahia maisha ndani ya klabu hiyo na ataongeza mkataba.

"Nafikiri kwa wakati huu ana furaha," alisema Matic, ambaye yeye mwenyewe aliongeza mkataba mapema mwezi huu akinukuliwa na Stats Perform News.

# Lampard: Ni kazi ngumu kufuzu Ligi ya Mabingwa



**LONDON,** England

FRANK Lampard anaamini itakuwa ngumu kwa Chelsea kujihakikisha nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, licha ya kujikita nafasi ya tatu Jumanne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Bao la kipindi cha kwanza la Olivier Giroud lilitosha kuona Chelsea wakiifunga Norwich City 1-0 pale kwenye dimba la Stamford Bridge, wakijivuta pointi nne zaidi ya Leicester City na Manchester United, ambao wapo nafasi ya nne na tano wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

Lakini vijana hao wa Lampard wana mechi dhidi ya Liverpool na Wolves ili kumaliza msimu huu na kujihakikishia kumaliza kwenye nne bora.

Na kocha huyo wa Chelsea anaamini timu yake bado ina mtihani mgumu mbele yake ili kuweza kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

"Nimekuwa nikiendelea kuzungumza kuhusu akili na kujituma na sitaki kufikiria zaidi vitu ambavyo bado haujavipata.

"Unapokuwa na mchezo unaokuja dhidi ya Liverpool ugenini na Wolves nyumbani, ni wapinzani wazuri sana," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunatakiwa kuelekeza akili yetu kwenye mechi moja baada ya nyingine, kujiandaa vizuri zaidi, kuonyesha mtazamo mzuri kama tulivyofanya dhidi ya Norwich, kwani mechi hizi ni ngumu kwetu.

# DYBALA KUOGA NOTI JUVENTUS




**TURIN,** Italia

PAULO Dybala anatarajiwa kuwa mchezaji wa pili anayelipwa fedha nyingi zaidi ndani ya klabu ya Juventus, kwa mujibu wa Tuttosport.

Dybala alikuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, mwaka jana, lakini alibakia hapo na kufurahia maisha mjini Turin akiwa na msimu wa kuvutia.

Na sasa, mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina anatarajiwa kupata zawadi yake nono ya kuongezewa mkataba wake.

Huku mkataba wake ukitarajiwa kufikia mwishoni mwaka 2022, Dybala anakaribia kusaini mkataba mpya na Juventus utakaomweka hapo hadi mwaka 2025, gazeti la Tuttosport limeeleza.

Nyota huyo sasa atakuwa mchezaji wa pili anayelipwa fedha nyingi zaidi Juve, nyuma ya mshambuliaji Cristiano Ronaldo.

Dybala amefunga mabao 17 na kutoa pasi za mwisho nane katika mechi 41 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu.



# *Klopp alalama Manchester City kusamehewa*

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpoool, Jurgen Klopp amesema Jumatatu "haikuwa siku nzuri" baada ya Manchester City kufanikiwa kwa rufani yao ya kupinga kufungiwa miaka miwili kucheza mashindano ya Ulaya baada ya kuvunja kanuni ya usawa ya matumizi ya fedha kwenye usajili wa wachezaji, FFP.

Shirikisho la Soka Ulaya (Uefa), liliifungia Man City miaka miwili na faini ya euro milioni 30, lakini Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo (Cas), ilifuta adhabu hiyo na kupunguza faini hadi euro milioni 10.

Na Klopp kocha wa zamani wa Borussia Dortmund alisema baada ya maamuzi hayo: "Siihofii Liverpool. Kwa uhakika nina furaha kwa kushinda taji la Ligi Kuu kwa sababu halitakuwa jambo rahisi kwa siku za usoni kama kuna vitu vitabadilika.

"Naipenda FFP kwa sababu inatupa njia nzuri. Lakini sina uhakika ni namna gani inafanya kazi, kwani ninachojua inatupa sisi njia ya kufanya kazi na usawa, kitu ambacho kwangu sina tatizo nacho.

"Kama hivyo, sasa tunatakiwa kubadili hilo, kwani kwa hali hii siku za usoni zitaonyesha jinsi ambavyo ilitakiwa kufanya kazi. Katika soka, tunajua kwamba, Jumatatu hii haikuwa nzuri kwa soka.

"Haikuwa siku ambayo hatukutakiwa kusherehekea, 'Oh, kuanzia sasa kila mmoja anaweza kutumia fedha nyingi kadri anavyotaka."

Alielezea kwamba, kwa kuondolewa adhabu hiyo kwa Man City, inamaanisha kwamba klabu nyingine zitaweza kufanya lolote na hakuna hatua itakayochukuliwa.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SUAREZ: UBINGWA LALIGA BARCA IJILAUMU YENYEWE

●●● Tuliliachia litukimbie wenyewe, hatutakiwi kutafuta sababu ya huruma...

**BARCELONA,** Hispania

LUIS Suarez amesisitiza Barcelona wanatakiwa kujilaumu wenyewe kwa kuachia ubingwa wa LaLiga kuponywa, akisema kushinda taji hilo kwa sasa haiwezekani.

**Huku mechi mbili zikiwa zimesalia, Barca wamepitwa pointi nne na wapinzani wao na vinara, Real Madrid.**

Kikosi hicho cha Quique Setien kilionekana kuwa kwenye njia nzuri ya kulibeba taji hilo msimu huu, lakini walipoteza pointi katika mechi zake tatu zilizopita kati ya saba.

Suarez amesema Barcelona wanatakiwa kujilaumu wao wenyewe kwa kuliachia taji hilo, akikubali kwamba haiwezekani kushinda ingawa Madrid bado hawajajihakikishia kabisa kulitwaa.

"Kwenye Ligi unatakiwa kujiangalia wewe mwenyewe, tuliliachia litukimbie wenyewe," alisema akiliambia gazeti la Mundo Deportivo.

"Tunajua kwamba, tulijitegemea sisi wenyewe, na hatutakiwi kutafuta sababu ya huruma.

"Kwa sasa fahari yetu kwa Barca, tunatakiwa kushinda mechi mbili zilizobaki, na kuelekeza akili yetu kwenye kombe ambalo tunaweza kulipigania, ambalo ni Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Tukipigana kwa kiwango ambacho kimetufanya kuwa kwenye klabu hii, tunaweza kupambana na yeyote. Kushinda inaweza kuwa gharama kubwa kwetu, hivyo tunatakiwa kuwa makini na kucheza kwa kujituma kuhakikisha tunaweza kulibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu na mlinzi, Gerard Pique wamekuwa watu kutoka ndani ya Barcelona ambao wamepaza sauti zao wakisema maamuzi ya hivi karibuni ya VAR yamekuwa yakiibeba Real Madrid.

Hata hivyo, Suarez amekataa kutumia sababu hiyo, badala yake amelaumu timu kutoka sare dhidi ya Sevilla, Celta Vigo na Atletico Madrid.

"Hili wazo kwamba, tulitakiwa kushinda mechi dhidi ya Sevilla, na hata Vigo, na lilikuwa pigo kwa Atletico Madrid, lakini tungeweza kupata ushindi," alisema mshambuliaji huyo.

"Kufikiria huruma ya VAR ni kitu kigumu. Ndio, Gerard na rais walitoa malalamiko yao hadharani, lakini nafikiri hilo si jambo muhimu kwetu, kwani kuna timu kama Athletic (Bilbao), Getafe pia wao waliathirika na VAR, lakini hawakulalamika."

## ZISIKUPITE

### MAITLAND KUONDOKA ARSENAL

AINSLEY Maitland-Niles amebainisha kwamba kipindi chake cha kucheza Arsenal kimefikia mwisho, huku klabu za England na Ujerumani zikiwania saini yake. ***(The Sun)***

### AJAX, CELTIC KWA DIANGANA

AJAX na Celtic ni miongoni mwa klabu zinazowania kumsajili Grady Diangana huku West Ham wakipambana kujaribu kushawishi abakie klabuni hapo kwa msimu mwingine. ***(The Sun)***

### PSG YAMTA RASHFORD

KLABU ya Paris Saint-Germain inawania kumsajili Marcus Rashford, ambaye 'yupo tayari kusikiliza' ofa yoyote, lakini Manchester United wamepanga ada ya pauni milioni 100 ili kumwachia straika huyo. ***(Daily Star)***

### HENDRY ATUA OOSTENDE

KLABU ya Celtic ya Scotland imebainisha kwamba, Jack Hendry amekamilisha uhamisho wa mkopo kwenda Oostende. ***(Scottish Sun)***

### COUTINHO LULU ARSENAL

KLABU ya Barcelona inaamini kwamba itamtoa kiungo wake, Philippe Coutinho kwa mkopo kipindi hiki cha majira ya joto, huku ikiripotiwa kwamba nyota huyo wa Brazil anawaniwa Arsenal na Newcastle. ***(Daily Mirror)***

### UMTITI KUPELEKWA ARSENAL

BARCELONA ipo tayari kumtoa kwa mkopo Samuel Umtiti anayewindwa na Arsenal kipindi hiki cha majira ya joto. ***(The Sun)***

### SPURS JICHO KWA WIGAN

KLABU ya Tottenham Hotspur imefanya mazungumza na Wigan Athletic juu ya mpango wa kumsajili kiungo chipukizi, Alfie Devine kwa pauni 500,000 kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Daily Mail)***

### OZIL AMTEGA ARTETA

MESUT Ozil anaonekana kwamba yupo tayari kufanya kazi chini ya kocha, Mikel Arteta baada ya kuposti kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Istagram kwamba 'yupo tayari'. ***(Daily Mail)***

### KAI HAAMBILIKI CHELSEA

KAI Havertz anayewaniwa na Chelsea anabainisha kuwa yupo tayari kujiunga na klabu hiyo, hata kama haitafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, kwa mujibu wa magazeti ya Uingereza. ***(Daily Star)***

### LAZIO JICHO KWA MORELOS

KLABU ya Lazio ya nchini Italia imemwweka straika wa Rangers, Alfredo Morelos kwenye orodha ya wachezaji wanaowania kuwasajili kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Scottish Sun)***

### HOJBJERG HUYO SPURS

NAHODHA wa zamani wa Southampton, Pierre-Emile Hojbjerg ameripotiwa kwamba anajiandaa kuhamia Tottenham Hotspur mwishoni mwa msimu huu. ***(Daily Mail)***

## HABARI MICHEZO

# TARIMBA AZIPIGIA DEBE TIMU NCHINI

**Na Faustine Feliciane**

MKURUGENZI wa Utawala na Udhibiti wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, ameyakumbusha makampuni ya michezo ya kubashiri matokeo kurudisha sehemu ya faida wanayopata kwa wananchi ikiwamo kudhamini timu za Ligi Kuu Bara na Ligi Daraja la Kwanza.

Akizungumza kwenye ofisi za gazeti hili jana, ikiwa ni ziara yake kwa vyombo vya habari kushukuru kwa SportPesa kupokelewa vema na kuungwa mkono tangu kuanza shughuli zake miaka mitatu iliyopita hapa nchini, Tarimba aliweka wazi makampuni ya ubashiri yanapata faida kubwa.

"SportPesa tunathamini kile ambacho tunakipata, faida ambayo tunapewa na Watanzania tunairejesha kwao, njia moja wapo ni pamoja na kudhamini klabu za Ligi Kuu, tumekuwa wadhamini wa Simba, Yanga na Namungo," alisema Tarimba na kuendelea,

**"Serikali inaweza ikaweka kipengele kwa makampuni yote kabla ya kupata leseni lazima wakubali kutoa sehemu ya faida yao kwa Watanzania kama ambavyo SportPesa tunafanya, timu zipo nyingi mpaka za Ligi Daraja la Kwanza," alisema Tarimba.**

Aliongeza lengo la SportPesa si tu kuona kampuni inakuwa kibiashara, lakini kuona michezo hapa nchini inakua na ndio sababu wanafurahia mafanikio ya timu wanazozidhamini.

"Timu zote tunazozidhamini zinafanya vizuri, hivi karibuni tutashuhudia mchezo wa fainali ya Kombe la Shirikisho Tanzania (FA Cup), na timu zote zilizoingia hatua hiyo zinadhaminiwa na kampuni yetu (Simba na Namungo), haya yote kwetu ni mafanikio," Tarimba alisema.

Aliongeza anawashukuru Watanzania na wadau wa mpira pamoja na serikali kwa kuwa sehemu ya mafanikio ya kampuni hiyo kwa muda wote tangu ilipoanza kutoa huduma zake hapa nchini.

"Tunawaahidi kuendelea kutoa huduma, lakini kuendelea kurejesha kwa jamii faida tunayoipata, kama nilivyosema lengo letu si tu kupata faida, lakini kuona michezo hapa nchini hususan mpira wa miguu unazidi kukua," alisema Tarimba.

**MSHINDI...**



Msemaji wa Klabu ya Simba, Haji Manara (wa pili kushoto) akimkadhi funguo na kadi ya gari, mshindi wa Promosheni ya Babalao, Didas Mmishi aliyeshinda zawadi ya gari aina ya Toyota Funcargo. Kushoto ni Meneja wa Kampuni ya Global Publishers, waandaaji wa promosheni hiyo, Abdallah Mrisho na Mhariri Mtendaji wa magazeti ya kampuni hiyo, Saleh Ally. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Yanga yawataka mashabiki 'kupotezea' kipigo*

**Na Adam Fungamwango**

MAISHA yaendelee! Yanga imewataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kusahau kipigo walichokipata dhidi ya watani zao, Simba na kuelekeza 'akili' katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizobaki ili kumaliza msimu kwenye nafasi ya pili.

Yanga ilichapwa mabao 4-1 na Simba na kutolewa kwenye mashindano ya Kombe la FA, ambayo bingwa wake atakata tiketi ya kupeperusha bendera ya Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema imekuwa ni bahati mbaya kwao kupoteza mchezo huo dhidi ya Simba ambao umewafanya wapoteze nafasi ya kuiwakilisha nchi katika michuano ya kimataifa msimu ujao.

Bumbuli alisema Yanga imepoteza mechi lakini haijapoteza heshima ya klabu yao ambayo inarekodi ya kushinda mataji mbalimbali.

"Tumepoteza mchezo, tumepoteza nafasi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho, lakini hatujapoteza thamani ya klabu ya Yanga na heshima yetu, ndiyo maana ya kauli yetu ya daima mbele nyuma mwiko, yale yote yameshapita, tunaganga yajayo, lengo letu ni kushika nafasi ya pili katika Ligi Kuu," alisema Bumbuli.

Kiongozi huyo amewataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kushikamana na kuendelea kujenga hamasa kuelekea katika msimu mpya.

"Kwanza lengo ni kushinda mechi zote zilizosalia ili tushike nafasi ya pili kwa ajili ya heshima ya klabu yetu, huku mengine yote yakifanyiwa kazi kwa ajili ya msimu ujao wa ligi, pamoja na usajili, lakini kuna maandalizi ya Siku ya Mwananchi ambayo tayari yameshaanza," Bumbuli alisema.

Baada ya Yanga kutolewa katika mashindano ya Kombe la FA, tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika imekwenda kwa Namungo FC ambayo imetinga fainali kutokana na Simba tayari kuwa na tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika.

## 'Killer Man' kurudisha dansi

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI wa muziki wa dansi, ambaye ni Mkurugenzi wa Bendi ya Waluguru Original, Deogratius David 'Killer Man, amesema anatamani kuona mji wa Morogoro unatamba kwenye dansi kama enzi za zamani.

Alisema, miaka ya 60 hadi 70, Morogoro ulikuwa ni miongoni mwa miji, iliyovuma kwa muziki wa dansi, lakini baadaye hali hiyo ikabadilika baada ya wakongwe wa muziki wa dansi kufariki dunia.

"Mji wa Morogoro ulitamba ukiwa na wanamuziki maarufu wengi kama Mbaraka Mwishehe na wengine, lakini sasa sivyo, nami ninatamani sana enzi hizo zirudi na ninajitahidi kufanya hivyo," alisema 'Killer Man'.

Alisema njia anayoitumia ni kushirikiana na wanamuziki wake kuandaa nyimbo, ambazo zinavutia mashabiki wa muziki wa dansi wakiwamo wa nje ya Morogoro, ambao amedai kuwa wameanza kumiminika kuishuhudia.

Alisema, bendi yake imetunga wimbo wa kutangaza vivutio vya Morogoro, uitwao 'Morogoro Yetu' na umeanza kusikika katika vituo vya redio mjini humo, ikiwa ni moja ya mkakati wake wa kurudisha Morogoro kwenye dansi.

Alisema, wimbo huo utabeba albamu mpya ya mwaka huu yenye nyimbo za 'Mwanzo wa Mapenzi, Cha Kupewa, Ngalile Mwanangu Ndole, Supu na Nataka Nilewe' iko mbioni kuzinduliwa.

## Machomane matumaini kibao Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Machomane United ya Kisiwani Pemba umesema lengo lao kubwa ni kuona timu hiyo inabaki katika Ligi Kuu Zanzibar licha ya sasa kuwa kwenye hatari ya kushuka daraja.

Timu hiyo leo itashuka dimbani kuvaana na Jang'ombe Boys, ambayo nayo iko katika 'hali tete' katika mchezo utakaopigwa kwenye Uwanja wa Mau A.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Machomane, Omary Iddi, alisema timu hiyo imejiandaa kupata alama tatu katika mchezo wa leo na kurejesha matumaini ya kubaki katika ligi hiyo msimu ujao.

Iddi alisema anajua mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani huku akiongeza kuwa anawaheshimu wapinzani wake Jang'ombe Boys ambayo nayo imejipanga kurekebisha makosa yao.

" Tumebakia na mechi ngumu, tunajua Jang'ombe Boys inaundwa na wachezaji wenye uzoefu katika ligi hii, hivyo hatutarajii mchezo kuwa rahisi kwetu, tunajipanga kukutana na ushindani na sababu kubwa timu zote ziko kwenye nafasi mbaya katika msimamo," Iddi alisema.

Kiongozi huyo amewataka waamuzi kuzingatia sheria 17 za mchezo huo katika kipindi hiki cha lala salama ili timu itakayostahili ichukue ubingwa kwa halali na zile zinazopambana kubakia kwenye Ligi Kuu nazo zibakia kwa haki," aliongeza Iddi.

# Michezo

Alhamisi Julai 16, 2020

Nipashe




Suarez: Ubingwa LaLiga Barca ijilaumu UKURASA 22

ASANTENI...



Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas (kushoto), akitoa ufafanuzi namna kampuni hiyo inavyoinua sekta ya michezo nchini kwa Mhariri wa Michezo wa Nipashe, Isaac Kijoti (kulia), wakati wa ziara yake katika Kampuni ya The Guardian Ltd, kushukuru SportPesa kupokelewa vema. Kulia kwake ni Meneja Uhusiano SportPesa, Sabrina Msuya, Meneja Rasilimali Watu wa The Guardian Ltd, Emmanuel Matondo, Mhariri Msanifu Mkuu Nipashe, Theodatus Muchunguzi pamoja na waandishi wa gazeti hilo. **HABARI UK. 23. PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# *TFF yamtetea Morrison, yaiachia Yanga iamue*

## Yamshangaa mwamuzi kumzuia kutoka nje ya uwanja, yasema hakuna sheria...

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI wadau wa soka nchini na mashabiki wa Yanga wakisubiri kusikia hatua itakayochukuliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kupitia Bodi yake ya Ligi (TPLB) kwa winga wa kimataifa wa klabu hiyo, Mghana Bernard Morrison kutokana na utovu wa nidhamu aliuonyesha kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Simba, chombo hicho kinachobeba dhamana la soka nchini, kimemtetea.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa Jumapili iliyopita na Simba kushinda mabao 4-1, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael alimtoa Morrison dakika ya 79 na nafasi yake kuchukuliwa na Patrick Sibomana, lakini winga huyo hakukaa katika benchi na badala yake kuamua kutoka moja kwa moja uwanjani na kuondoka.**

Wakati anatoka mwamuzi wa akiba alijaribu kumzuia na kumtaka kwenda kukaa benchi na wenzake, lakini Morrison aligoma na kuondoka, jambo ambalo limezua mjadala mzito kutoka kwa wadau wa soka pamoja na vyombo vya habari, huku baadhi ya wachambuzi wakidai ni kosa kisheria.

Hata hivyo, akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati akitangaza tarehe ya mechi ya fainali ya Ligi Daraja la Kwanza kati ya Gwambina FC ya mkoani Mwanza na Dodoma FC, Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo, alisema alichokifanya Morrison si kosa kisheria bali ni suala tu la utovu wa nidhamu. Kasongo alisema hakuna sheria inayomzuia mchezaji kutoka nje ya uwanja na kudai alimshangaa mwamuzi wa akiba katika mchezo huo alipokuwa anamzuia kutoka nje.

"Kiujumla hajafanya kitendo cha kiungwana, alipaswa kuheshimu mashabiki pamoja na benchi lake la ufundi, lakini alishindwa pia kuwaheshimu wachezaji wenzake na kuamua kutoka nje moja kwa moja, suala hilo litaamuliwa na Yanga wenyewe," alisema.

Aidha, Kasongo aliwataka wachezaji kuwa na nidhamu pindi wawapo uwanjani ili kujiepusha kupata lawama ambazo hazina maana kutoka kwa mashabiki wao.

Kuhusu fainali ya Ligi Daraja la Kwanza kati ya Gwambina FC ya mkoani Mwanza na Dodoma FC, Kasongo alitangaza kuwa itapigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

"Fainali ya kumpata Bingwa wa Ligi Daraja la Kwanza itachezwa Jumamosi hii, tunaomba wadau mbalimbali wajitokeze kwa wingi kushuhudia mchezo huo ambao utakuwa na ushindani mkubwa wikiendi hii," alisema Kasongo.

Mtendaji huyo alisema michezo ya timu zote ambazo zilishinda nafasi ya pili na ya tatu itachezwa kesho ambapo mchezo wa kwanza utaikutanisha Transist Camp FC dhidi ya Ihefu mechi ambayo itapigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, wakati timu ya Majimaji FC itaumana na Geita FC kwenye dimba la Majimaji mjini Songea, kabla ya timu hizo kurudiana Julai 22, mwaka huu ili kupata timu mbili ambazo zitapambana na timu zinazowania kubaki Ligi Kuu.

# Simba, Mbao FC mechi ya malengo

**Na Saada Akida**

TUNATAKA heshima! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Sven Vandenbroeck kuelekea mchezo wa ligi hiyo dhidi ya Mbao FC kutoka Mwanza utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Sven aliliambia gazeti hili jana anahitaji kupata pointi tatu katika mchezo huo ili kuendelea kuupa heshima ubingwa wa msimu huu wa 2019/20, ambao wameshautwaa.

Kocha huyo alisema baada ya mapumziko ya siku mbili, kikosi kilirejea kwenye mazoezi jana asubuhi na anaamini nyota wake watakuwa na nguvu mpya ya kusaka ushindi katika mchezo huo dhidi ya Mbao ambayo inahitaji pia pointi ili kujiondoa kwenye hatari ya kushuka daraja.

"Tunahitaji kumaliza ligi tukiwa na pointi nyingi, hivyo tunaenda kufanya kazi kuhakikisha wachezaji wanatafuta matokeo, tunajua Mbao FC wako katika hali mbaya, lazima waingia na nguvu," alisema Sven.

Naye nahodha wa Simba, John Bocco, alisema: "Mbao ni timu nzuri ingawa wako katika nafasi mbaya, hivyo watakuja kutafuta matokeo, lakini kwa upande wetu tunahitaji kukusanya pointi katika michezo yote iliyobakia," alisema Bocco.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >